**KILO** 88 dawa za kulevya zabambwa kwenye Prado

UKURASA 3



**HAKIMU** atoa ushahidi kwenye kesi dhidi ya kigogo wa NIDA

UKURASA 4


Wakuu someni ujumbe wenu huu!

BUFE

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

EWURA RASMI OPERESHENI KUSAKA 'VISHOKA' WAUNGANISHAJI UMEME

Usimamizi bora wa mapato waipatia Halmashauri Ilala Hati Safi miaka 5

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Juni 18, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA

ISSN 0856 • Na. 0580615

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745


# Tuhuma mpya zamwandama Ole Sabaya



**TAKUKURU** yathibitisha kuzipokea, yasema inazichunguza, kesi yake kutajwa leo....*Endelea Uk. 2*



Mfanyabiashara mdogo akiwa ameweka kibanda chake juu ya mfereji wa maji ya mvua, katika Barabara ya Nelson Mandela, eneo la Ubungo Riverside, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Fedha za TCRA, TPA, TASAC kuwekwa akaunti maalum BoT

UKURASA 2

UKURASA WA 4

## SAMIA ASHUSHA GHARAMA YA VIZIMBA SOKONI MORO

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameagiza kushushwa kwa bei ya pango kwa vibanda na vizimba vilivyopo ndani ya...

UKURASA WA 5

## RUGEMALIRA APANDA KORTINI KESI YA UHUJUMU UCHUMI

MKURUGENZI Mtendaji wa Kampuni ya VIP Engineering, James Rugemarila na Mwanasheria wa Independent Power Tanzania Limited...

## CHADEMA YAGOMEA RUZUKU YA BIL. 1/-

UKURASA 3

**MICHEZO** **MAYAY ATOA SABABU KUKUBALI KUKATWA TFF** UK. 24

**MAONI, KATUNI UK. 6**

# Tuhuma mpya zamwandama Ole Sabaya

**Na Allan Asack,** ARUSHA

WAKATI aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akitarajiwa kupandishwa tena kizimbani leo, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imesema imepokea malalamiko mapya kutoka kwa watu mbalimbali na inayachunguza.

Imesema iendapo tuhuma dhidi yake zitathibitika, itafungua mshtaka mengine mapya dhidi ya mshtakiwa huyo na wengine wanaodaiwa kuhusika.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Salum Hamduni, alisema wamepokea malalamiko kutoka kwa wananchi mbalimbali na kama uchunguzi wao utabaini Ole Sabaya na wenzake walitenda makosa hayo, watawafungulia mashtaka mengine.

"Suala lililopo mahakamani siwezi kulizungumzia kwa kuwa nitakuwa nimeingilia muhimili wa Mahakama.

"Lakini ninapenda kukueleza kuwa tumepokea malalamiko kutoka kwa watu mbalimbali na tukifanya uchunguzi wetu na tukabaini malalamiko hayo ni ya kweli, hatua nyingine za kisheria zitafuata ikiwamo kumfungulia mashtaka mengine," alifafanua.

Mkurugenzi huyo alipoulizwa kuhusu watu wengine wanaodaiwa kuunganishwa kwenye mashtaka mapya akiwamo Meya wa Manispaa ya Moshi, Juma Raibu, alisema kwa sasa hawezi kulizungumzia suala hilo kwa kuwa wapo katika hatua ya uchunguzi wa malalamiko hayo.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Kilimanjaro, Frida Wikesi, alithibitisha kuwa taasisi hiyo imepokea malalamiko dhidi ya Ole Sabaya na wenzake na wanayafanyia kazi na uchunguzi ukikamilika watatoa taarifa kwa vyombo vya habari.

"Ni kweli tumepokea malalamiko na tunayafanyia kazi, uchunguzi ukikamilika tutawapatia taarifa.

"Bado hatujamfungulia mashtaka mengine kwa kuwa tunaendelea kuchunguza tuhuma tulizozipokea kutoka kwa watu mbalimbali kama zina ukweli," Frida alisema.

Juni 15 na 17 mwaka huu, TAKUKURU ilinukuliwa na vyombo vya habari (siyo Nipashe) ilibainisha kuwa miongoni mwa tuhuma hizo, ni iliyotolewa na mfanyabiashara maarufu mjini Moshi, Elioth Lymo, aliyedai kuwa fedha zake kiasi cha Sh. milioni 25 zilichukuliwa Sabaya isivyo halali.

Ilidaiwa kuwa wapo baadhi ya watu wanatajwa kushirikiana na Ole Sabaya kufanya uhalifu akiwamo Meya wa Manispaa ya Moshi, Raibu, ambaye naye anachunguzwa na endapo uchunguzi utathibitisha kuwa anahusika, atafikishwa mahakamani.

Hata hivyo, meya huyo alinukuliwa jana na baadhi ya vyombo vya habari akikanusha tuhuma hizo kuwa siyo za kweli na hana ushirikiano na Ole Sabaya kufanya matukio hayo ya kiuhalifu.

Juni 4 mwaka huu, Ole Sabaya na wenzake walipandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha wakikabiliwa na makosa matano ya uhujumu uchumi, rushwa, kuongoza genge la uhalifu, utakatishaji wa fedha na unyang'anyi wa kutumia silaha.

Ole Sabaya, msaidizi wake na walinzi wake walifikishwa mbele ya mahakama mbili tofauti za Arusha kujibu mashtaka yanayowakabili.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine ni pamoja na msaidizi wake wa karibu Silvester Stanslaus, Enock Togolani, John Odemba, Daniel Gabriel na Waston Mwakomange.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsindikiza Balozi wa Uturuki nchini Tanzania, Mehmet Gulluoglu, baada ya mazungumzo yao, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Fedha za TCRA, TPA, TASAC kuwekwa akaunti maalum BoT

**Na Waandishi Wetu**

TAASISI ya WAJIBU imefanya uchambuzi wa mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha, ikibaini kuzingatiwa kwa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Imesema miongoni mwa mapendekezo ya CAG yaliyozingatiwa katika kukuza uwazi, uwajibikaji na utawala bora, ni uamuzi wa serikali kuweka kwenye akaunti maalum katika Benki Kuu (BoT) mapato ya Mamlaka ya Bandari (TPA), Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) na Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC).

Akiwasilisha uchambuzi wa WAJIBU kuhusu bajeti hiyo mkoani Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo na CAG mstaafu, Ludovick Utouh, alisema uamuzi huo umezingatia mapendekezo ya CAG katika ripoti yake ya mwaka 2019/20.

Utouh aliyewahi kuwa CAG kwa miaka minane kuanzia mwaka 2006, alikumbusha kuwa Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2019/20 iliyowasilishwa bungeni Aprili mwaka huu, ilibainisha kuwapo matumizi mabaya ya fedha za TPA huku mabilioni ya takriban Sh. bilioni mbili zikitumika kugharamia vikao vya bodi na watendaji wa TASAC.

"Mapato ya TPA, TCRA na TASAC kuanzia mwaka 2021/22 yatakuwa yakikusanywa na taasisi hizo kupitia mfumo wa GePG na kuingizwa kwenye akaunti za makusanyo (holding accounts) zilizopo Benki Kuu.

"Hii inaonyesha serikali imezingatia mapendekezo ya CAG katika ripoti yake iliyowasilishwa bungeni Aprili mwaka huu.

"Mfano, Ripoti ya CAG ilionyesha upotevu wa Sh. bilioni 3.93 kutokana na miamala ya udanganyifu katika Bandari ya Kigoma na Mwanza uliosababishwa na udhaifu wa mifumo ya ndani katika usimamizi wa malipo," Utouh alisema.

Mtaalamu huyo wa fedha alisema hoja nyingine ya CAG iliyozingatiwa wameiona katika mabadiliko ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Sura 418.

Utouh anafafanua kuwa mabadiliko hayo yatafanya mashirika yote ambayo yanamilikiwa na serikali moja kwa moja ama kupitia taasisi zake sasa kukaguliwa na (CAG).

"Mabadiliko hayo yatamwezesha waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha bungeni majibu kuhusu taarifa ya CAG baada ya CAG kuwasilisha taarifa yake.

"Utaratibu wa sasa unataka taarifa zote kuwasilishwa kwa pamoja katika kikao kimoja cha Bunge. Hii ilitokana na mabadiliko ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2013 ambayo hayakutekelezeka hadi sasa," alifafanua.

Utouh alisema uchambuzi wao pia umebaini hoja za CAG zimezingatiwa pia katika mabadiliko ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura 134 ambayo yatairuhusu serikali kudhamini kampuni au taasisi yoyote ya umma kukopa kiasi kisichozidi thamani ya hisa za serikali kwenye kampuni au taasisi husika baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mawaziri.

Utouh alisema kuwa uamuzi huo wa serikali unajibu hoja ya CAG kuhusu upungufu wa mitaji kwa mashirika yanayomilikiwa na serikali.

**MADENI HIFADHI JAMII**

Mkurugenzi huyo alisema uchambuzi wao pia umebaini bajeti inayopendekezwa imezingatia hoja ya CAG kuhusu hali ya mifuko ya hifadhi ya jamii nchini.

Anasema serikali kupitia bajeti hiyo inatarajia kulipa madeni inayodaiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii kwa kutenga fedha kwenye bajeti na kutumia utaratibu wa kutoa hatifungani maalum isiyo taslimu (non-cash special bonds) zitakazoiva kwa nyakati tofauti kuanzia miaka miwili hadi 25.

"Hii itasaidia kuyajumuisha madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii kwenye Deni la Taifa na kusaidia mifuko hiyo kufanya uwekezaji wa fedha hizo," alifafanua.

Utouh pia alisema serikali imefanyia kazi pendekezo la kuongeza mapambano dhidi ya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu wa mali za umma.

Alibainisha kuwa kila mwaka Ripoti za CAG zimekuwa zikitoa taarifa za upotevu wa mali za umma hasa kutokana na rushwa na udhaifu wa mifumo ya ndani wa serikali katika ngazi zote na taasisi zake.

Utouh alisema taasisi yao imeona bajeti inayopendekezwa inalenga kukuza uchumi na kuongeza pato la mwananchi mmoja mmoja, hivyo kupunguza umaskini nchini.

Alisema wanaamini mapendekezo yaliyotolewa na wadau mbalimbali, ikiwamo taasisi yao, yatazingatiwa na kufanyiwa kazi na serikali na Bunge katika kukamilisha utayarishaji wa bajeti hiyo ya mwaka 2021/22 inayotarajiwa kuwa ya Sh. trilioni 36.33.

■ **Imeandikwa na Sanula Athanas na Enock Charles**

# CHADEMA yazikataa bil. 1/- za ruzuku



Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe

**Na Mwandishi wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema kuwa kimekataa kupokea ruzuku ya Sh. bilioni moja, kwa kile walichodai kutoridhishwa na uchaguzi wa mwaka 2020.

Akizungumza na wananchi wa Mtwara katika ziara ya kukijenga na kukiimarisha chama hicho, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, alisema watakijenga chama hicho kwa nguvu za wanachama na wadau wengine.

"Tumesema kwanza tunajenga chama kitakachokuwa cha kujitegemea, hatutaki ruzuku hata senti tano kutoka serikalini... kila siku wanapigia simu "Mbowe unajua tangu uchaguzi mkuu mpaka sasa hivi mna Sh. ngapi," juzi amenipigia kuwa tuna Sh. bilioni moja, njooni mchukue hela, ni hela zenu hizi," alisema.

"Nikamwambia huu urafiki wetu na Chama Cha Mapinduzi (CCM), umeanzia wapi, kama kweli mna huruma na sisi (CHADEMA) tupeni serikali yetu, hiyo ruzuku kaeni nayo," alisema.

Alisema zamani walikikabili chama hicho kwenye ruzuku kwa kuisimamisha au kuwa imeliwa na kuita Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) akague, na kwamba sasa wanajenga chama kitakachojitegemea, hivyo siyo uamuzi rahisi.

Mbowe alitolea mfano wa malezi ya mtoto kuwa; "Hata mwanao nyumbani anataka maziwa unampa, nusu saa anataka soda unampa, anataka chips mayai unampa, saa sita anakula, saa tisa anataka tena kula chakula kingine unampa, saa 11 anataka kula unampa... hayo siyo mapenzi ni kumwaribu mtoto, utalea mtoto zezeta asiyejua kujitegemea wala kutafuta."

"Nasi kama chama cha upinzani ni hivyo hivyo, ili tuweze kujitegemea, lazima tukatae vya bure, tunakubalije ruzuku wakati tunasema uchaguzi mzima nchi nzima uliibiwa. Tukisema leo Kanda ya Kusini tuna madiwani sijui kumi na wangapi. Chama chetu kilikuwa na madiwani nchi nzima 1,294 na mwaka huu tulikuwa na uwezo wa kukamata zaidi ya madiwani 2,000 hadi 3,000."

Naye, Mwenyekiti wa Vijana wa CHADEMA (BAVICHA), John Pambalu, alisema chama hicho ni cha siasa na siyo kikundi cha watu, na kwamba ajenda ya Katiba Mpya ni ya Watanzania.

"Hitaji la Katiba Mpya siyo hisani ya watawala bali hitaji la Watanzania," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake (BAWACHA), Catherine Ruge, alisema Mkoa wa Mtwara una hazina kubwa ya gesi na madini, lakini hali ya umaskini na miundombinu bado ni duni, huku zao la korosho likichangia fedha nyingi za kigeni kwa taifa.

# Kilo 88 dawa za kulevya zabambwa kwenye Prado

**Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), imekamata kilo 88.27 za dawa za kulevya aina ya heroin na methamphetamine zikiwa kwenye gari aina ya Toyota Prado.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Kamishna Jenerali wa DCEA, Gerald Kusaya, alisema dawa hizo zilikamatwa Juni 2, mwaka huu, baada ya maofisa waliokuwa doria wakishirikiana na wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kulitilia shaka gari hilo na kuanza kulifuatilia.

"Dereva wa gari baada ya kugundua anafuatiliwa, alilitelekeza na kukimbia eneo la Kimara Korogwe, Dar es Salaam. Baada ya upekuzi wa kisheria kufanyika ndani ya gari hilo, kulipatikana mifuko mikubwa mitatu aina ya sandarusi ndani yake ikiwa na pakiti 12 za dawa za kulevya aina ya heroin," alisema.

Kusaya aliongeza kuwa: "Dawa hizo zilikuwa na uzito wa kilo 12.25 pamoja na kontena za pastiki 73 ndani yake kukiwa na dawa aina ya methamphetamine zenye uzito wa kilo 76.02. upelelezi wa shauri hili unaendelea."

Kadhalika, Kusaya alitoa onyo kwa watu wanaofanya biashara ya usafirishaji na watumiaji wa dawa za kulevya kuacha, vinginevyo wataishia katika mikono isiyo salama.

"Ninawaambia mamlaka iko macho saa 24, ama zao ama zetu dhidi yao. Ni vyema wakatafuta biashara nyingine ya kufanya, tuko macho hatulali," alisema Kusaya.

Aliongeza kuwa DCEA iko vizuri kwenye mapambano ya matumizi ya dawa za kulevya, kwamba kwa viwango vya kimataifa Tanzania ipo kwenye kiwango cha asilimia 90 katika udhibiti.

Wakati huohuo, Kusaya alisema Juni 26, kila mwaka, Tanzania huungana na mataifa mengine kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya Duniani.

Alisema katika maadhimisho ya mwaka huu, kitaifa yatafanyika jijini Dodoma katika viwanja vya Nyerere Square, mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

'Kauli mbiu ya mwaka huu inasema 'Tuelimishane Juu ya Tatizo la Dawa za Kulevya, Kuokoa Maisha'. Kaulimbiu hii inaelekeza jamii inatakiwa kujua ukweli juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya, ili isijiingize katika matumizi ya dawa hizo," alisema.

Alisema maadhimisho yataanza Juni 24 na yatatanguliwa na maonyesho ya shughuli mbalimbali za udhibiti wa dawa za kulevya zinazofanywa na taasisi za serikali, asasi za kiraia na watu binafsi.



## Sheria kulinda faragha za watu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema inatarajia kuja na sheria mbili ikiwamo ya kukusanya na kutunza taarifa za watumiaji kutokana na kuwa hatarini.

Hatua hiyo inalenga kuweka mifumo wa kuainisha ni taarifa zipi zinazochukuliwa kwa mwananchi na kwa malengo gani, ili kuepuka kuchukua taarifa zisizostahili.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, katika Mkutano wa Wizara hiyo, taasisi zake na wahariri wa vyombo vya habari jijini hapa.

Alisema katika utafiti mdogo uliofanywa na wizara hiyo kwa Wilaya ya Kinondoni, imebaini taarifa za watu zilizochukuliwa na taasisi mbalimbali zipo wazi na hazina faragha, jambo ambalo ni hatari kwa usalama.

"Sasa muda si mrefu tunakuja na sheria mbili, lakini ieleweke haina lengo la kukumiza mtoa huduma, ila ina lengo la kumlinda mtumiaji. Katika utafiti wetu mdogo kwa Wilaya ya Kinondoni tumebaini taarifa za walioumwa na hata alichokisema daktari kipo wazi.

"Si hilo tu hata kama uliomba hati ya kusafiria taarifa zako pia zipo wazi, lakini hata kwa matukio ya uhalifu unawezaje kuhusianisha suala la dini au kabila la mtu.... ndio maana sasa tunakuja na sheria hizi ili kulinda faragha ya kila Mtanzania, tutaweka mifumo ya taasisi zichukue taarifa zipi," alisema.

Alisema wizara inaendelea na mchakato wa utungaji sheria hizo kwa manufaa ya Watanzania katika kulinda faragha zao.

Waziri huyo alisema pia wizara ipo kwenye mchakato wa kufanya mapitio na maboresho ya sheria na kanuni zinazosimamia sekta hiyo na kufunga sheria na kanuni mpya ili kuweka mazingira bora ya ushindani na udhibiti.



Mkurugenzi Mtendaji wa Songas Tanzania, Anael Samuel, akizungumza na Balozi wa Norway Tanzania, Elisabeth Jacobsen, katika uzinduzi wa ripoti ya miaka 50 ya ushirikiano katika nishati ya umeme, iliyoandaliwa na ubalozi huo, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Norfund kupitia Globeleq ni mmoja wa wanahisa wa Songas pamoja na TPDC na TANESCO. Songas imekuwa ikizalisha 20% ya nishati ya umeme nchini, tangu mwaka 2004. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Hakimu atoa ushahidi kesi kigogo NIDA

**Na Kulwa Mzee**

HAKIMU Mkazi Mkuu, Thomas Simba, jana alipanda kizimbani kutoa ushahidi katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Dickson Maimu na wenzake wanne.

Simba alitoa ushahidi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rashid Chaungu.

Katika ushahidi wake, Hakimu Simba alidai Desemba 6, 2016 alidai kuwa alishuhudia mkataba wa mauziano ya gari kati ya mshtakiwa aliyekuwa Ofisa Usafirishaji wa NIDA, George Ntalima na Kampuni ya Messonm Limited. Alidai kuwa mauziano hayo ya gari aina ya Heacher lenye namba za usajili T791 DEE rangi nyeupe yalifanywa na pande zote mbili huku yakishuhudiwa na Hakimu Simba.

Anadai alishuhudia mkataba huo wa mauziano ya gari kwa thamani ya Sh. milioni 34 na mnunuzi kwa niaba ya Kampuni ya Messonm, John Msangi alipa fedha hizo zote Desemba 6, 2016. "Makubaliano yalitiwa saini na pande zote, mnunuzi na muuzaji niliwashuhudia na wote niliwaona," alidai Hakimu Simba.

Wakili wa Serikali, Zacharia Ndaskoi, akimwongoza shahidi huyo, aliomba kutoa mkataba huo kama kielelezo mahakamani. Kutokana na ombi hilo hakukuwa na pingamizi, hivyo mahakama ilipokea na kuuweka kama kielelezo namba 44.

Washtakiwa katika kesi hiyo, mbali na Maimu, ni Meneja Biashara Aveline Momburi, Ntalima, Mkurugenzi wa Sheria, Sabina Raymond na Xavery Kayombo. Washtakiwa walishtakiwa mwaka 2016 kwa mara ya kwanza wakikabiliwa na mashtaka 55 yakiwamo ya kusababisha hasara ya Sh. bilioni 1.175, kughushi, kuwasilisha nyaraka za uongo kwa mwajiri na matumizi mabaya ya madaraka.

Wanadaiwa kutenda makosa hayo kati ya Januari 15 hadi 19, 2010 katika Makao Makuu ya NIDA, Kinondoni mkoani Dar es Salaam.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 17/06/2021

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **ALHAMIS tarehe 18-06-2021** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka MBWENI kuelekea BUNJU, gari hilo lenye namba za usajili: **T 175 DFN / T 168 DFF.**
2. **Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 18.00 |
| Upana | - | mita | 2.82 |
| Kimo | - | mita | 4.6 |

3. Njia itakayotumika: **MBWENI hadi BUNJU kupitia MOROGORO.** ***Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)***

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*


## Samia aagiza kushushwa bei vibanda, vizimba sokoni Moro

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameagiza kushushwa kwa bei ya pango kwa vibanda na vizimba vilivyopo ndani ya Soko Kuu la Kingalu la mjini Morogoro.

Pia ameagiza kupangwa upya utaratibu wa wafanyabiashara wadogo, kwa ajili ya kufanya biashara sokoni hapo. Maagizo hayo yaliwasilishwa na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, wakati akizungumza na wafanyabiashara wadogo.

Wafanyabiashara hao waligoma kuuza bidhaa zao ndani ya soko hilo na kupanga chini nje, kwa madai ya kukosa wateja, huku wakitaka wenzao wanaouza katikati ya mji kuondolewa.

Hivyo, Rais Samia aliwaagiza watendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kushusha bei za pango katika soko hilo, ili wafanyabiashara waweze kumudu gharama na kupata faida ya shughuli wanaofanya.

Alisema bei ya awali ya Sh. 300,000 kwa vibanda (fremu) za chini itashushwa hadi Sh. 100,000, vibanda vya juu kutoka Sh. 200,000 hadi Sh.50,000 na vizimba kushuka kutoka Sh. 20,000 hadi Sh. 10,000 kwa mwezi.

"Bei hizi zitadumu kwa muda wa miaka miwili, na baada ya hapo tutaangalia na kukubaliana kuongeza bei ya pango au vinginevyo," alisema Shigela.

Mbali na hilo, Shigela alipiga marufuku askari wa Jeshi la Akiba, marufu kama mgambo kutojihusisha na shughuli zozote za operesheni, ikiwamo zinazohusu kuwakamata watu katika Mkoa wa Morogoro.

Pia aliagiza wafanyabiashara waliopo katika maeneo ya barabarani kupangiwa utaratibu wa kufanya biashara zao eneo la soko kwa nje, sambamba na kupiga marufuku kutozwa fedha au ushuru wowote kwa pikipiki na bajaji wanaoingia katika soko hilo.

Pia alionya uongozi wa Manispaa ya Morogoro kutotegemea mapato kutoka katika chanzo cha soko, kwani serikali iliamua kujenga wenyewe kama ruzuku kwa wananchi.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wafanyabiashara akiwamo, Salma Saud, alishukuru hatua hiyo ya Serikali na kuomba kuwekwa kwa utaratibu wa bidhaa za aina moja katika eneo la wazi la chini ambazo hazitaingiliana na zile za ndani, ili kuepuka muingiliano wa biashara na waliopo ndani kwenye vizimba.

Meya wa Manispaa ya Morogoro, Pascal Kihanga, alisema maagizo hayo yatafanyiwa kazi, kwamba yatasaidia kuwa na wafanyabiashara wengi katika soko hilo tofauti na sasa.

**HABARI KITAIFA**

## Sheria ajira kwa wageni kuboreshwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali inaboresha Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Na. 1 ya mwaka 2015 ili kuondoa vikwazo kwa wawekezaji na kulinda ajira za Watanzania.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Ukonga (CCM), Jerry Silaa.

Mbunge huyo alisema Aprili 6, mwaka huu, wakati Rais Samia Suluhu Hassan akiapisha viongozi wa serikali, alitoa kauli ya kusikitishwa kwa jinsi wawekezaji wanavyokwamishwa kwenye vibali vya kazi na kutoa maelekezo ya serikali kutengeneza utaratibu mzuri ili kusaidia watu hao kutopata mkwamo.

Aidha, alisema kauli hiyo imepokewa kwa furaha na wawekezaji wengine na imechukua sura mpya katika sekta ya uwekezaji nchini lakini kuna baadhi ya maeneo imechukuliwa tofauti na baadhi ya wafanyabiashara wasio waadilifu ambao wameanza kuleta wafanyakazi kwenye maeneo ya wazawa kama vile marubani kwenye kampuni binafsi za ndege. Alihoji serikali ina mkakati wa kutekeleza maagizo ya Rais katika kuwaondolea vikwazo na urasimu wawekezaji kupata vibali vya kazi na kuendelea kutekeleza matakwa ya sheria hiyo ambayo inalinda ajira za Watanzania kwenye maeneo ambayo wana uwezo wa kufanyia kazi.

Waziri Majaliwa alisema kwa sasa wanatengeneza sheria na kuboresha ili kuwafanya wawekezaji wasikwazwe. "Lakini Watanzania wasipoteze fursa ya kuajiriwa, kwa hiyo matumizi ya fursa hizo vibaya nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tunasimamia vizuri na hasa marekebisho ambayo tunayafanya kwenye uwekezaji yenye nia njema hasa kutoa fursa kwa Watanzania, nitoe wito kwa wawekezaji kuja nchini kuwekeza maana rasilimali zipo," alisema.

Alibainisha uwekezaji nchini ni mkakati mpana ambao unahamasisha ujenzi wa uchumi kwa kukaribisha wawekezaji wa nje na ndani ya nchi kwenye uwekezaji na wanao watu wanaowaamini kushiriki katika shughuli zao za uendeshaji wa uwekezaji wao.

Alieleza serikali imeweka sheria ya uwekezaji ambayo haipanui wigo mpana ukapoteza fursa ya Watanzania kushiriki kwenye uwekezaji huo ikiwamo ajira.

"Tunachukua hatua gani ya wale ambao wanatumia nafasi hii vibaya, serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu bahati nzuri hili jambo lipo ofisini kwangu na tunalisimamia vizuri," alisema. Aliwahamasisha wawekezaji wote kuja nchini kuwekeza kwenye sekta mbalimbali kwa fursa zilizopo, pia Watanzania kushiriki kwenye uwekezaji huu ili na wao wawe sehemu ya ujenzi wa uchumi kupitia uwekezaji.

# Hatima viwanda visivyofanya kazi mikononi mwa Baraza la Mawaziri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Mawaziri linatarajiwa kutoa uamuzi kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi ili wapewe watu wenye uwezo wa kuviendesha.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ndanda (CCM), Cecil Mwambe.

Mbunge huyo alisema serikali ya Tanzania imepitia awamu sita za uongozi na kwamba ya kwanza ilijikita kwenye kujenga viwanda kwa ajili ya kuboresha ajira na uzalishaji, ya tatu ilibinafsisha ili kuviboresha na kuongeza ajira na ya tano ilikuja na sera ya ujenzi wa viwanda ili kuongeza ajira na uzalishaji.

"Viwanda vilivyobinafsishwa na serikali ya awamu tatu havifanyi kazi iliyokusudiwa vikiwamo vya korosho. Nini msimamo wa serikali kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi iliyokusudiwa?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Majaliwa alisema serikali iliunda tume ambayo iliongozwa na Msajili Hazina akiwamo Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanya mapitio ya viwanda vyote vilivyobinafsishwa vikiwamo vya korosho.

"Serikali tumechukua viwanda vyote ambavyo kwa sasa vinafanyiwa uchambuzi na serikali na timu inayoongozwa na Msajili wa Hazina ili kupeleka taarifa kwa Baraza la Mawaziri ambalo litatoa uamuzi wa kutoa viwanda hivyo kwa watu wenye uwezo wa kuviendesha," alisema.

Alibainisha kuwa lengo ni kutoa viwanda hivyo kwa watu ambao wana uwezo kwa sababu serikali ya awamu ya sita inasisitiza sekta binafsi lazima iwe karibu na serikali ili kupanua wigo wa uchumi wa nchi.

"Nasikitika kuna baadhi waliopewa viwanda hivyo hawakufanya vizuri sana, serikali ilichofanya ni kuchukua viwanda vyote ambavyo havikufanya vizuri.

"Tukipata watu ambao wana nia kwa masharti ambayo tutaweka ili kuendeleza mkakati wetu wa viwanda, nikuhakikishie viwanda ambavyo havifanyi kazi vilisharatibiwa na vitatolewa kwa watu wenye uwezo wa kuendesha," alisema.

Alitoa wito kwa watu wenye nia ya kuwekeza kwenye viwanda kuwa tayari kupokea baada ya baraza hilo kufanya uamuzi ili waviendeshe kwa ufanisi mkubwa.

MISAMAHA YA KODI

Katika hatua nyingine, Majaliwa ameliambia bunge kuwa lazima bidhaa au misaada inayotolewa kwa taasisi ikiwamo za dini zikidhi matakwa ya serikali.

Alizitaka taasisi ambazo zinapata misamaha ya kodi kupitia misaada mbalimbali kutoka nje ya nchi kuhakikisha wanaeleza nini wanataka kuleta nchini ili kipate msamaha huo.

Aidha, amesema ni lazima bidhaa au misaada inayoletwa ikidhi matakwa ya serikali kwamba kifanyike kitu ambacho kimekusudiwa au kinachotakiwa.

Waziri Mkuu alisema serikali imeweka utaratibu wa kutoa misamaha kwa baadhi ya taasisi zinazotoa huduma za jamii ambazo zinalenga kuisaidia serikali katika utoaji wa huduma hizo.

"Uzoefu ambao tumeupata serikalini ni kwamba watu wanaweza kuomba msamaha lakini anachokileta nchini sio kile alichokiombea msamaha hivyo kunakuwa na hatua ndefu ambazo mwingine husema kwamba hii ni urasimu wa serikali hapana," alisema.

"Tumejipanga vizuri kwa kutoa maelekezo bandarini, viwanja vya ndege kwenye mipaka yetu nchini ili wateja wetu wapate huduma za haraka ikiwamo na wanaopata misamaha," alisema Majaliwa wakati akijibu swali la Mbunge wa Kilolo (CCM), Justine Nyamoga.

Katika swali lake, Nyamoga alisema taasisi za dini zimekuwa zikikumbwa na adha kubwa na vikwazo vingi na urasimu wakati wa kushughulikia misamaha ya kodi wanapopata vifaa au misaada mbalimbali kutoka nje ya nchi.

Alisema hali hiyo imesababisha wakati mwingine vifaa hivyo kukaa muda mrefu bandarini na kuingia tatizo la kutozwa gharama za kuhifadhi ambazo mwisho wake wanashindwa kuvitoa na kuhoji kauli ya serikali kuhusu tatizo hilo.



Mfanyabiashara James Rugemalira akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, baada ya kesi inayomkabili ya uhujumu uchumi, kutajwa kwenda kuisikiliza Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Rugemalira apanda kizimbani kesi uhujumu uchumi

**Na Kulwa Mzee**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kampuni ya VIP Engineering, James Rugemarila na Mwanasheria wa Independent Power Tanzania Limited (IPTL), Joseph Makandege, wamepanda kizimbani kuendelea na kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili badala ya mshtakiwa mwenzao, Habinder Sethi, kuachiwa huru.

Washtakiwa hao walifika jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakati kesi inayowakabili ilipotajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai mahakamani kwamba kesi ilikuja kwa ajili ya kutajwa na upelelezi haujakamilika, hivyo aliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Mahakama ilikubali kuahirisha kesi hiyo hadi Julai Mosi kwa ajili ya kutajwa na washtakiwa walirudi rumande.

Baada ya Sethi kuachiwa huru kwa masharti, Rugemalira na Makandage walibaki kwenye kesi hiyo.

Rugemarila, ambaye ni mmiliki mwenza wa zamani wa IPTL anadaiwa kutenda makosa hayo mkoani Dar es Salaam na nchi za Afrika Kusini, Kenya na India.

Anakabiliwa na mashtaka 12 yakiwamo ya utakatishaji fedha, miongoni mwa mashtaka hayo yapo ya kula njama, kujihusisha mtandao wa uhalifu, kughushi na kutoa nyaraka za kughushi na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, kutakatisha fedha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh. 309,461,300,158.27.

Inadaiwa kati ya Oktoba 18, 2011 na Machi 19, 2014 jinini Dar es Salaam, walikula njama katika nchi za Afrika Kusini, Kenya na India ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Mwanasheria Makandege, anakabiliwa na mashtaka matano likiwamo la kuisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 980,000.

Makandege aliondoa maombi yake ya kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Mei 6, mwaka huu, na Rugemarila hakuwahi kuandika barua kuomba kukiri makosa yake.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi wachukue tahadhari ya corona

**MAPEMA** wiki hii, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, aliwataka Watanzania kuchukua tahadhari dhidi ya corona kwa kuvaa barakoa wanapokuwa kwenye mikusanyiko.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa kuchukua tahadhari ikiwamo kunawa mikono mara kwa mara, kutumia vitakasa mikono, kuepuka misongamano na safari zisizo za lazima.

Alisema nchi jirani kama Uganda na nyingine zinakabiliwa na corona, kwamba ni ngumu kujua nani ameambukizwa au la, ndiyo maana ni muhimu kuchukua tahadhari.

Jana serikali ya Afrika Kusini ilieleza kuwapo kwa wimbi la tatu la kirusi cha corona, kiasi cha kuongeza masharti ikiwamo muda kutoka nje ukiwa mwisho ni saa 4 usiku, na sehemu za starehe zikiongezewa masharti mapya.

Nchini Uganda kuna zuio la mikusanyiko na kusafiri kutoka wilaya moja kwenda nyingine, huku hospitali zikielemewa wagonjwa na idadi ya vifo ikiongezeka.

Taarifa ya jana inaeleza kuwa wapo waliopata corona wenye umri wa miaka 20 tofauti na awali ugonjwa huo ulipoanza kundi lililokuwa hatarini ni lenye umri wa miaka 35 kuendelea, pamoja na wenye magonjwa yasiyoambukiza kama moyo, kisukari, shiniki zo la damu na Ukimwi.

Bado baadhi ya wananchi wanachukulia rahisi suala la corona kwa kuachana na tahadhari zote muhimu, na hilo linaonekana kwenye maeneo ya mikusanyiko ya watu wengi kama sokoni, nyumba za ibada na biashara kama Kariakoo na kwingine.

Nchini takwimu zilizopo ni za Machi mwaka jana, na hadi sasa serikali imepokea taarifa ya kamati ya ushauri ya corona, ambayo pamoja na mambo mengine, imeshauri nchi kukubali chanjo, lakini iwe ni hiari.

Kwa sassa katika shughuli zote za Rais Samia Suluhu Hassan, anakuwa amevaa barakoa na msisitizo mkubwa ni kila mtu aliyepo eneo hilo kuhakikisha amevaa.

Hizi ni jitihada za wazi kwa kuwa Tanzania siyo kisiwa na tunapakana na nchi nane kati yake sita zimeweka wazi takwimu za kila siku za maambukizi na vifo.

Aidha, huduma za usafiri wa mabasi, maji na anga zinaendelea kama kawaida, huku kukiwa na mwingiliano wa watu kwenye maeneo ya mipakani.

Hivyo, tahadhari inayotolewa na Waziri ambayo awali ilisisitizwa na Rais Samia kwa maneno na vitendo inapaswa kutiliwa maanani kwa kuwa madhara ya corona ni makubwa sana.

Kuna wakati madaktari walieleza kuwa bado wale waliougua corona wanabaki na madhara ya muda mrefu mwilini, jambo linaloonyesha kuwa licha ya kupona bado unaweza kujikuta katika hali nyingine ngumu ya kujiuguza maradhi mengine.

Tunafikiri ni muhimu sana wananchi wakasisitizwa kuvaa barakoa kila mahali ikiwamo kwenye ofisi zote za serikali na binafsi pamoja na kwenye mhimili muhimu wa Bunge ambao umekusanya wawakilishi wa wananchi.

Bila kuchukua tahadhari hasa kuvaa barakoa kuna uwezekano wa kusambaza ugonjwa huo na kuleta madhara hasa kwa watu ambao kinga yao ya mwili iko chini.

Pia, tunashauri serikali kuharakisha utafiti wa aina ipi ya chanjo itawafaa Watanzania wanaotaka kuchanjwa, ili kutoa uhuru wa kuendelea na shughuli zao ikiwamo kwenda kwenye nchi ambazo huwezi kuingia bila kuchanjwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hoja ya Morogoro iwe fursa kutengea maeneo Machinga

Na Sabato Kasika

**KILIO** cha muda mrefu cha wajasiriamali wamachinga, ni cha kutaka halmashauri ziwajengee masoko yakiwa na miundombinu yote muhimu, ili waondokane na mtindo wa kupanga biashara katika maeneo yasiyo rasmi kwa shughuli zao.

Hata hivyo, ni kama kilio ambacho hakijasikika, kutokana na uhalisia kwamba wanaendelea kufanya biashara zao kwenye maeneo yasiyo rasmi na wakati mwingine inasababisha usumbufu kwa watu wengine.

Kuna wakati wanaziba njia za waendao kwa miguu, kwa kupanga bidhaa zao na 'kuvamia' vituo vya daladala wakivigeuza kuwa masoko yao. Ni hali ambayo kwa ujumla wake inazaa usumbufu kwa wengine.

Zao la kero hiyo imefanya baadhi ya halmashauri kuwaondoa kwa nguvu kwenye maeneo yasiyo rasmi, lakini baadaye wanarejea na kuendelea na biashara zao kama kawaida, huko walikoondolewa.

Hatua hiyo, inaweza kusababishwa na mambo mawili. Kwanza, ni kwamba huenda hawajatengewa maeneo rasmi ya kufanyia biashara zao ambayo yameboreshwa, au maeneo yapo, lakini wahusika wanakaidi.

Wenye majibu sahihi kwenye jambo hili ni viongozi wa halmashauri, manispaa na wamachinga wenyewe kwamba maeneo hayo hawataki kwenda au masoko hayana miundombinu rafiki.

Vuta nikuvute ya viongozi wa halmashauri na wamachinga ya uhamishaji wa kutoka maeneo waliopo, imekuwa ikisababisha vurugu na udhalilishaji ambao ungeweza kuepukika kama kila upande ungetimiza wajibu wake.

Mfano mmojawapo ni tukio la mwanzo wa wiki, lililotokea mjini Morogoro baada ya mgambo kutaka kuwaondoa wamachinga kwa nguvu, kwenye eneo walilokuwa wakifanya biashara na kusababisha vuta nikuvute.

Vuta nikuvute hiyo imemsababisha Rais Samia Suluhu Hassan, kuwafuta kazi mkuu wa wilaya na mkurugenzi wa halmashauri baada ya kuchukizwa na anavyoshughulikia suala la wamachinga hao.

Ingependeza kama yaliyotokea Morogoro, yatakuwa ni fursa kwa viongozi wa halmashauri na manispaa nchini, kuchukua hatua za kutenga maeneo ya wamachinga, yakiwa na miundombinu yote muhimu ili wasipate kisingizio.

Inaelezwa kuwa, wamachinga wa Morogoro walitengewa eneo lilelo nje, lisilofikiwa na wateja, ndipo wakaamua kurejea mjini, lakini viongozi wa wilaya wakaingilia kati kuwaondoa kwa njia ambayo haikumfurahisha Rais.

Wamachinga hutajwa kuwa wana umuhimu katika kukuza pato la taifa, kwa kuwa sekta yao ina wajasiriamali milioni tatu na laki moja na kwamba, takwimu za viwanda na biashara zinaonyesha kuwa sekta ya viwanda vidogo na biashara zimetengeneza ajira, kukuza uchumi na kuondoa umaskini nchini.

Pia watu walioajiriwa katika sekta hiyo ni asilimia 23.4 ya nguvukazi ya taifa na imechangia asilimia 27 katika Pato la Taifa.

Pia, serikali inawatambua umuhimu wao katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo. Hivyo, badala ya viongozi kutumia nguvu kubwa kuwaondoa wamachinga kwenye maeneo waliopo sasa, wenye mamlaka wakune vichwa kuhakikisha wanajenga masoko ya kutosha na kisha ndio wawahamishe.

Mtindo wa kuwahamisha kwa awamu na kuacha wengine wakiendelea na biashara kwenye maeneo waliondolewa, unasababisha malalamiko na mwisho wa siku, wanarudi kuungana na wenzao.

Si vibaya hayo ambayo yametokea Morogoro yakageuzwa kuwa fursa ya kukaa na kutafakari jinsi ya kuboresha mazingira ya biashara za wamachinga, ili wasisumbue watu mitaani lakini waondokane na kero ya kutimuliwa ovyo.

Moja ya malalamiko yao makubwa ambayo yanasababisha wasiende kwenye masoko waliotengewa, kwani ni ukosefu wa huduma muhimu zikiwamo za vyoo, maji, usafiri na wateja, hali inayowafanya wazidi kubaki mitaani.

Ukosefu wa huduma hizo kwenye maeneo wanayofanyia biashara zao, umekuwa hoja yao kubwa, ambayo wamekuwa wakitamani ifanyiwe kazi kwanza kabla ya kuhamishwa maeneo waliopo sasa.

Kuimarisha uchumi bila kuchafua mazingira nalo ni jambo muhimu, hivyo ingekuwa vyema pakajengwa masoko ya kutosha, yenye huduma zote muhimu kibinadamu na kibiashara ambazo wamachinga na jamii yote mahali hapo wanayahitaji.

# Mbowe ampongeza Rais Samia kuachiwa Uamsho

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kusikia ombi na kilio cha wengi dhidi yamashekhe wa Uamsho walioachiwa jana.

Akizungumza jana katika ziara zake mkoani Mtwara, alisema; "Tunamshukuru Rais Samia na wenzake wote ambao hatimaye wamesikia kauli na vilio vya watu wengi wakitaka haki ya watu hawa."

Alisema maumivu yao binafsi na familia zao ambazo ziliathirika kwa kiasi kikubwa, na kwamba kuna mambo yanayopaswa kutojirudia Tanzania.

Mbowe alisema ni muhimu hali ya utengamano katika taifa ukawa ni jambo la kudumu, na kutoruhusu watoto wa kitanzania wa dini, chama chochote wakakamatwa pasipo haki na kurundikwa magerezani.

"Kama sheria zetu ndiyo zinasema hivyo hizo ni batili na ndiyo sababu tunataka Katiba Mpya itakayotoa uhuru, haki na maendeleo ya watu wetu," alisema.

Aidha, alihoji aliyewaweka ndani ni nani na kwasababu gani na hasara iliyopatikana nani anastahili kuwalipa fidia na aliyehusika anachukuliwa hatua gani.

APONGEZA POLISI

Aliwapongezi polisi wilayani Masasi kwa ulinzi na ushirikiano mkubwa kwenye vikao, msafara na shughuli zao za kichama.

"Sitatenda haki kama sikutoa shukrani za kipekee kabisa kwa Jeshi la Polisi, wametupa ushirikiano sana Masasi, wamehakikisha usalama wetu wa msafara, vikao na mikutano."

# Onyo matumizi dawa za kutoa mimba

**Na Mary Geofrey**

JAMII imeonywa kuepuka matumizi holela ya dawa za kutoa mimba, uzazi wa mpango na za kupunguza maumivu, bila kufuata ushauri wa wataalamu wa afya kwa kuwa zina madhara makubwa ikiwamo ugumba. Ushauri huo ulitolewa jijini Dar es Salaam na Rais wa Chama cha Wafamasia, Fadhili Hezekia, wakati akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Wafamasia yaliyofanyika katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Alisema kila dawa ina madhara katika mwili wa binadamu, hivyo wataalamu hutambua ni dawa kiasi gani na kwa wakati apewe mgonjwa ili asipate madhara hayo.

Hezekia alisema matumizi ya dawa holela hasa za uzazi wa mpango zinachanganya mfumo wa homoni na matokeo yake kusababisha uvimbe na hatimaye ugumba.

"Athari za matumizi ya dawa zinatokana na uelewa mdogo kwa jamii hivyo siyo sahihi jamii kutumia dawa bila kufuata ushauri wa daktari hata kama ni za miti shamba," alisema Hezekia.

Alisema kwa matumizi ya dawa za maumivu siyo sahihi kwa sababu kila ugonjwa una chanzo, hivyo mgonjwa anaweza kudhani anaumwa mgongo kumbe ana tatizo la figo.

Kuhusu matumizi ya dawa za uzazi wa mpango kiholela, alisema zinasababisha madhara katika mwili wa mwanamke na hivyo kusababisha ugumba.

Mkurugenzi Mtendaji wa (MNH), Prof. Lawrence Museru, alisema kazi kubwa wanayofanya madaktari ni kuhakikisha dawa sahihi zinapatikana kwa wakati na kutumia kwa masharti sahihi.

Alisema MNH katika kudhibiti matumizi holela ya dawa, wameanzisha utaratibu mpya wa kutoa dawa za kila siku kwa wagonjwa waliolazwa badala ya kutoa dozi nzima ili kuepuka uharibifu.

# TTB yahamasisha utalii mikoa kusini

**Na Zuhura Zukheir, IRINGA**

BODI ya Utalii Tanzania (TTB), imewataka wadau mbalimbali wa utalii kushirikiana na serikali kutangaza vivutio vilivyoko kusini mwa Tanzania.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Meneja wa Mikutano na Matukio wa TTB, Irene Mvile, wakati wa kikao cha mikakati ya kutangaza vivutio vya kusini mwa Tanzania kilichofanyikia mjini hapa.

Alisema wadau wa utalii kwa kushirikiana na serikali kwa pamoja wanaweza kutekeleza mkakati huo wa kukuza utalii pamoja na pato la taifa kwa ujumla kwa kuongeza idadi kubwa ya watalii kutembelea vivutio vilivyopo.

Kwa mujibu wa Mvile, wadau wa kusini wanavitambua vivutio vilivyopo na namna ya kuvitangaza, hivyo wanapaswa kutoa ushirikiano wa kutosha kwa serikali ili kufanikisha jambo hilo.

Akifungua kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, alisema mikakati ya TTB ni ya kutangaza vivutio vya kitalii vilivyopo kusini ili kuchochea kukuza uchumi wananchi na kuleta maendeleo kwa haraka kutokana na ongezeko la watalii litakalokuwapo.

"Niwapongeze sana TTB kwa jitihada za kutangaza vivutio vilivyopo Kusini serikali ya mkoa wa Iringa ipo pamoja na nyie katika kuhakikisha tunaweka mazingira rafiki kwa watalii watakaofika tunakarabati uwanja wa ndege wa Nduli na tunatamani hadi kufika mwakani tuanze kupokea wageni wengi watakaotembelea vivutio vyetu," alisema Sendiga.


## NOTISI / TANGAZO

**CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER,LEGENDS AUCTION MART LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, MUDU COMPANY LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, SALEI AUCTION MART LTD** kwa mamlakatuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| NO | JINA LAMDAIWA | TAWI ALILOKO PA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMNA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | FATUMA MSOMA KIULA | TEMEKE | AMIRI OMARI LUPATU | NYUMBA | KICHANGANI | 16-07-2021 NA KUENDELEA |
| 2 | NEEMA NASON SANGA | AGGREY | ADAM ISSA HASSAN | NYUMBA | MSINGWA-BONYOKWA TABATA- KIMANGA | 12-07-2021 NA KUENDELEA |
| 4 | DANIEL JAMES CHONGERA | AGGREY | DANIEL JAMES CHONGERA | NYUMBA | LUMUMBA PANGANI | 09-07-2021 NA KUENDELEA |
| 5 | MAGRETH STANLEY MWALUSAMBA | AGGREY | ELITRUDA ISDORY ASENGA | NYUMBA | MBEZI LUIS | 06-07-2021 NA KUENDELEA |
| 6 | ABDALLAH AHMAD MUHIDIN | TEMEKE | ABDALLAH AHMAD MUHIDIN | NYUMBA | TEGETA ' A' | 1-07-2021 NA KUENDELEA |
| 7 | MWANNE HASSAN SULEIMAN | TEMEKE | MWANNE HASSAN SULEIMAN | NYUMBA | MAMBOLEO-SANDALI TMK 038090 | 02-07-2021 NA KUENDELEA |
| 8 | MOHAMED ALLY ABDALLAH | TEMEKE | ZUHURA ZAHARANI HAMISI | NYUMBA | MAJIMATITU C-KIBONDE MAJI | 09-07-2010 NA KUENDELEA |
| 9 | ELINEEMA EMMANUEL KALALU | AGGREY | ELINEEMA EMMANUEL KALALU | NYUMBA | MBAGALA KUU MBAGHARIBI | 06-07-2021 NA KUENDELEA |
| 10 | MARIAM ALLY SHAMBE | AGGREY | MONICA ADAMS NDAJI | NYUMBA | UGINDONI-KIGAMBONI | 13-07-2021 NA KUENDELEA |
| 12 | WITGRACE ZEADIA NKYA | AGGREY | WITGRACE ZEADIA NKYA | NYUMBA | MKURANGA | 08-07-2021 NA KUENDELEA |
| 13 | MARIA GREGORY MKABAIRI | AGGREY | ZAINABU ALMAS | NYUMBA | MSUMI | 13-07-2021 NA KUENDELEA |
| 14 | JONATHAN AMAN ZAKAYO | AGGREY | AMAN BRAYAN ZAKAYO | NYUMBA | LUGURUNI-UBUNGO | 02-07-2021 NA KUENDELEA |
| 15 | JAFARI ATHUMAN JARIBU | MAIN | ASHA SAIDI KIBAVU | NYUMBA | MBAGALA-JUHUDI | 22-07-2021 NA KUENDELEA |
| 16 | JOSEPH JAILOS MALEMA | MBEYA | JOSEPH JAILOS MALEMA | NYUMBA | MTAAA WA BOMBAMBILI KATA YA MWAKIBETE | 2/7/2021 NA KUENDELEA |
| 17 | MOHAMED MIRAJI HUSSEIN | MBEYA | KIBONA AMBAKISYE KIBONA | NYUMBA | UYOLE-MBEYA | 4/7/2021 NA KUENDELEA |
| 18 | AMOS DAUD MUBOMBEGE | MBEYA | AMOS DAUD MUBOMBEGE | NYUMBA | MTAAA WA MWAMBENJA KATA YA IGANZO | 5/7/2021NA KUENDELEA |
| 19 | EZEKIEL WATSON KAJUNI | MBEYA | EZEKIEL WATSON KAJUNI | NYUMBA | CHIMALA | 02/07/2021 NA KUENDELEA |
| 20 | BARAKA BITON MKWAMA | MBEYA | BARAKA BITON MKWAMA | NYUMBA | CHIMALA | 06/07/2021 NAKUENDELEA |
| 21 | AMBELE JACOB MWAKASENDO | MBEYA | EMMANUEL DAVID NKALA | NYUMBA | TUKUYU | 10/07/2021 NA KUENDELEA |
| 22 | MICHAEL SAIMON MWAMWIMBE | MBEYA | STEVEN GEOFREY MWAKABUKU | NYUMBA | KIWIRA - MPANDAPANDA | 14/07/2021 NA KUENDELEA |
| 23 | GEITA JOSEPH NDELWA | MBEYA | GEITA JOSEPH NDELWA | NYUMBA | ILOMBA - KAGERA | 18/07/2021NA KUENDELEA |
| 24 | JOSEPH JAILOS MALEMA | MBEYA | BEATRICE JOSEPH MASAWE | NYUMBA | MWAKIBETE | 22/07/2021 NA KUENDELEA |
| 25 | FORTUNATUS ARON RUTAKINIKWA | MBEYA | FORTUNATUS ARON RUTAKINIKWA | NYUMBA | UYOLE - HASANGA | 26/07/2021 NA KUENDELEA |
| 26 | MAGETA GENERAL SERVICES LTD | BUGURU NI | SUKULU MAGETA | NYUMBA | TUANGOMA-KIGAMBONI | 03/07/2021 NA KUENDELEA |
| 27 | ELIZABERTH JOHN MTUI | ARUSHA | ELIZABERTH JOHN MTUI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | ARUSHA(USA RIVER-NGARESERO) | 03/07/2021 NA KUENDELEA |
| 28 | BONIFACE NDEWARIO NNKO | ARUSHA | BONIFACE NDEWARIO NNKO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | ARUSHA(USA RIVER-NGARESERO) | 05/07/2021 NA KUENDELEA |
| 29 | MARY BALTAZARY SHAYO | ARUSHA | MARY BALTAZARY SHAYO | NYUMBA | ARUSHA(SOKONI-ENGOSENGIU) | 10/07/2021 NA KUENDELEA |
| 30 | ONANSIA FELIX LEMA | ARUSHA | ONANSIA FELIX LEMA | NYUMBA | ARUSHA (TERRATI-MBUGA YA CHUMVI) | 7/7/2021 NAKUENDELEA |
| 31 | BEATRICE MOSES LEYARO | ARUSHA | BEATRICE MOSES LEYARO | NYUMBA | ARUSHA (BANGATA) | 9/7/2021 NAKUENDELEA |
| 32 | GLORIA OBEDI MUNISI | MOSHI | REMMY OBEDI MUNISI | NYUMBA | MTAA WA SADALA – WILAYA YA HAI | 05/07/2021 NA KUENDELEA |
| 33 | HELLEN HUMPHUREY SHANGO | MOSHI | HELLEN HUMPHUREY SHANGO | NYUMBA | MTAA WA ORMELILI – WILAYA YA HAI | 05/07/2021 NA KUENDELEA |
| 34 | AMINA HAMISI MKONDO | MOSHI | AMINA HAMISI MKONDO | NYUMBA | KATA YA PASUA MTAA WA MATINDIGANI – WILAYA YA MOSHI MJINI | 06/07/2021 NA KUENDELEA |
| 35 | MARISELINA JOSEPH MUNISHI | MOSHI | MARISELINA JOSEPH MUNISHI | NYUMBA | KATA YA RAU MTAA WA KARIWA CHINI - WILAYA YA MOSHI MJINI | 06/07/2021 NA KUENDELEA |
| 36 | LILIAN FELIX RIMOI | MOSHI | ROBERT LUCAS MINJA | NYUMBA | KISHUMUNDU – WILAYA YA MOSHI VIJIJINI | 07/07/2021 NA KUENDELEA |
| 37 | EMMANUEL TIMOTHY KABORA | AGGREY | EMMANUEL TIMOTHY KABORA | NYUMBA | MBWENI JKT, KINONDONI MUNICIPALITY, DARES SALAAM PLOT NO. 180, BLOCK 4 | 02/07/2021 NA KUENDELEA |
| 38 | SALEH ALLY MOHAMED | AGGREY | SALEH ALLY MOHAMED | NYUMBA | MZINGA B,TUANGOMA DSM | 08/07/2021 NA KUENDELEA |
| 39 | RAJABU MOHAMED MUOMBWA | AGGREY | RAJABU MOHAMED MUOMBWA | NYUMBA | KISEWE,YANGE YANGE,DSM | 09/07/2021 NA KUENDELEA |
| 40 | MUSTAPHA ABDALLAH ATHUMAN | AGGREY | MUSTAPHA ABDALLAH ATHUMAN | NYUMBA | KISEWE,YANGE YANGE,DSM | 09/07/2021 NA KUENDELEA |
| 41 | MAKONGORO MGABO NYAMHOZA | AGGREY | MWAJUMA MAKONGORO MATUTU | NYUMBA | VINGUNGUTI,MIEMBENI,DSM | 06/07/2021 NA KUENDELEA |
| 42 | OMARI SAID OMARI | AGGREY | MIZE MASOUD HASSAN | NYUMBA | MIKWAMBE TUANGOMA | 2/07/2021 NA KUENDELEA |
| **43** | COSMAS BRIAN MUSHI | AGGREY | COSMAS BRIAN MUSHI | NYUMBA | MBEZI MSUMI | 2/07/2021 NA KUENDELEA |
| **44** | EDSON KAPONKO | AGGREY | EDSON KAPONKO | NYUMBA | GOROKA "B" TOANGOMA | 2/07/2021 NA KUENDELEA. |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; **tupigie simu no.0682981090/0765387832/0759648448/0674821287/076867236707149399 33**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

## Gondwe akoshwa msaada wa elimu

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE nane zimepatiwa msaada wa Sh. milioni 43.8 ambapo tatu kati ya hizo kutoka Wilaya ya Temeke na tano za Wilaya ya Ulanga mkoani Morogoro.

Msaada huo umetolewa na Benki ya MMB, huku serikali ikiitaja benki hiyo kama kinara wa usaidizi katika utatuzi wa changamoto kwenye sekta za elimu na afya nchini.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe, wakati akipokea msaada wa mabati 576 yenye thamani ya Sh. milioni 18, kutoka NMB kwenda kwa shule za msingi Yombo Dovya, Faraja na Toangoma zilizopo wilayani mwake, kutoka kwa Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard.

Akizungumza wakati wa kupokea msaada huo, kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Yombo Dovya, Gondwe alibainisha kuwa, NMB imedumisha utamaduni chanya wa kujitoa, mara nyingine bila kuombwa, kutatua changamoto, kusapoti sera ya elimu bure, ambako serikali inatumia zaidi ya Sh. bilioni 3.5 kwa shule za wilaya yake tu.

Alibainisha Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan inatumia takribani Sh. bilioni 1.8 kwa shule za sekondari na Sh. bilioni 1.7 kwa msingi kwa mwaka, ambazo zinaweza kuwa hazitoshi, lakini uungwaji mkono inaopata kutoka kwa wadau wa elimu hasa NMB, umefanikisha maboresho ya mazingira ya kufundisha kwa walimu na kujifunza kwa wanafunzi.

"Hii Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii (CSR), ya NMB ni nzuri na ni jambo kubwa mno mnafanya. Mmekuwa vinara wa kusapoti jitihada za serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, tena mara nyingine mmefanya hivyo bila kusubiri kuombwa kusaidia katika wilaya yetu na Tanzania kwa ujumla," alisema Gondwe, aliyefichua kuwa ukongwe na uchakavu wa shule nyingi wilayani mwake, umeongeza uhitaji wa misaada.

Akaongeza kuwa, uthibitisho mwingine wa namna NMB inavyojitoa kustawisha sekta za elimu na afya, ni uamuzi wa benki hiyo kuunda timu maalum iliyopita mashuleni, hospitalini, zahanati na vituo vya afya wilayani Temeke, kukagua maeneo yanayohitaji usaidizi, sambamba na kuona matumizi ya misaada iliyokwishatolewa.

Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, aliishukuru Serikali pamoja na viongozi na walimu wa shule mbalimbali wilayani Temeke na Tanzania kwa ujumla, kwa kuichagua NMB kuwa mshirika sahihi katika utatuzi wa changamoto za elimu.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Yombo Dovya, Salum Gawaza, alisema shule yake iliyoanzishwa mwaka 1995, hivi sasa ikiwa na wanafunzi 2,270 na walimu 48, imekuwa na changamoto nyingi zinazotokana na uchakavu wa vyumba vya madarasa, Ofisi na miundombinu, na kwamba msaada wa NMB unaenda kuzipunguza, huku akiwataka wadau zaidi wa elimu kufuata nyayo za benki hiyo.

Wakati huo huo, Benki ya NMB kupitia Meneja wa Kanda ya Mashariki, Dismas Prosper, imekabidhi misaada yenye thamani ya Sh. milioni 25.8 kwa shule mbalimbali wilayani Ulanga mkoani Morogoro, yakiwemo mabati 234 na kofia zake 14, mbao 248, misumari kilo 100 na madawati 150.

Msaada huo, ulipokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Ngollo Malenya, kwa niaba ya uongozi wa shule za msingi Namgezi, Kwiro, Mbasa, Mahenge na Sekondari ya Lupilo.

# Waziri ataka makandarasi kuwafichua maofisa wapenda rushwa kwenye zabuni

**Na Joseph Mwendapole,** MWANZA

SERIKALI imewataka makandarasi kutaja majina ya maofisa wa serikali wanaowaomba rushwa ili wapate zabuni za miradi ya ujenzi ili watu hao wachukuliwe hatua.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho, alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa mashauriano baina ya Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) na makandarasi mbalimbali wa Kanda ya Ziwa.

Alisema uzoefu umeonyesha kuwa mkandarasi anapopewa zabuni kwa rushwa, anashindwa kukamilisha mradi kwa wakati na kwa ubora unaotakiwa, hivyo kuna umuhimu wa kushirikiana kutokomeza vitendo hivyo.

"Tupeni taarifa za watumishi wanaowaomba rushwa na sisi tutawalinda kwa sababu tunajua mnashindwa kuwataja kwa kuhofia kwamba mtakosa zabuni zinazokuja. Rushwa inaleta athari kubwa sana kwa hiyo tunapaswa kushirikiana kwa karibu," alisema.

Chamuriho aliwataka makandarasi hao kuungana ili kupata uwezo wa mitaji na weledi wa kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi badala ya kazi kubwa za ujenzi zinazotumia mabilioni ya fedha kufanywa na wageni.

Alisema serikali itafurahi kuona uwezo wa makandarasi wazalendo ukiimarika kwa kuwa wataweza kushindana na makandarasi wageni, hivyo kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi na fedha nyingi kubaki nchini kufanya kazi zingine.

"Acheni ubinafsi mfanye kazi kwa ubia, mkiungana ndipo mtapata uwezo wa kimitambo na utaalamu wa kushindana na wenzetu wa nje kwasababu hata hao wa nje mnaona wanafanyakazi kubwa kubwa hawako mmoja mmoja wengi ni kwasababu wameungana na kupata nguvu," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya CRB, Mhandisi Consolatha Ngimbwa, alimshukuru waziri akisema makandarasi wana imani kubwa kwamba kuwepo kwake kwenye wizara hiyo kutaleta ustawi kwao na kupiga hatua katika shughuli za sekta nzima ya ujenzi.

"Sisi makandarasi tuna imani kubwa na wewe na tunakuombea sana ili utimize majukumu yako kwa ufanisi zaidi maana umekuwa bega kwa bega na sisi licha ya kuwa na majukumu mengi ofisini kwako.

"Naomba nikukumbushe tumekaa hapa tunasubiri ahadi yako uliyotoa kule Mbeya kwamba utatoa tamko kuhusu matumizi ya 'force account'. Mwaka 2018 serikali ilisema iliamua kutumia utaratibu huo baada ya kuona bei zetu ziko juu sana lakini sasa tumeshatoa mafunzo na tuko tayari kufanya kazi na serikali kwa bei ndogo," alisema.

Alisema CRB iliamua kuanza kutoa mafunzo maalum kwa makandarasi kwa ajili ya kujaza zabuni tangu mwaka 2018 wamekuwa wakiwapa kozi hizo kwenye mikoa ya Morogoro, Arusha, Njombe, Dar es Salaam, Bukoba, Mwanza kwa ajili ya kuwatayarisha makandarasi waingie kwenye ushindani wa miradi ya serikali.

"Makandarasi walishiriki mafunzo kwa wingi na kwa uhakika wako tayari kufanya hizo kazi na mfano mzuri ni jengo letu la Dodoma wakati ule linawekewa jiwe la msingi. Rais wa awamu ya tano, Hayati John Magufuli, alifurahishwa na bei ambazo makandarasi wetu walitoa na alitaka tuendelee kutoa bei nafuu," alisema.




Naibu Msajili wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Mhandisi David Jere, akitoa mada kuhusu changamoto zinazoathiri ukuaji wa makandarasi, wakati wa mkutano wa mashauriano wa makandarasi mbalimbali wa Kanda ya Ziwa, jijini Mwanza jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Hali ya udumavu Iringa yamshtua RC

**Na Francis Godwin, IRINGA**

KIWANGO cha udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano mkoani Iringa ni asilimia 47 licha ya kwamba ni moja ya mikoa inayoongoza kwa uzalishaji wa mazao ya chakula.

Kutokana na tatizo hilo, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, ameagiza kufanyika kwa tathmini ya haraka kwenye halmashauri zote ili kujua hali halisi katika utekelezaji wa kitaifa wa lishe.

Sendiga alitoa agizo hilo jana katika ukumbi wa Mlandege kwenye kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mkataba wa lishe.

Alisema suala la tathmini ya lishe mkoa linapaswa kufanyika kuanzia ngazi za mitaa, vijiji hadi mkoa kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wanaume katika familia.

Pia alisema shughuli za utekelezaji wa mpango lishe mkoa zinapaswa kufanyika kwa uhakika pamoja na halmashauri kutenga na kutoa fedha za lishe kwa wakati kama inavyotakiwa. Alisema kila mkurugenzi wa halmashauri ndani ya mkoa anapaswa kuhakikisha anawajibika katika nafasi yake na asiwapo mtendaji wa serikali anakuwa kikwazo katika suala hilo.

Pia aliagiza vikao vyote vya halmashauri kuhakikisha ajenda ya lishe inakuwa ya lazima.

Naye Ofisa Lishe kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mariam Nakuwa, aliwataka wadau wa mkoa wa Iringa kuona jukumu la lishe linapewa kipaumbele zaidi.

Alisema pamoja na mkoa wa Iringa kuwa na changamoto ya lishe ndio mkoa wenye wadau wengi kulinganisha na mikoa mingine. Aliahidi kushughulikia suala la halmashauri kuchelewesha au kutoa fedha za lishe kama ilivyoagizwa.

Aidha, alisema waziri mwenye dhamana ameahidi kuanza kuwa makini katika uhakiki wa taarifa zinazotolewa na taarifa hizo zitolewe kwa wakati zaidi .

Awali, Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa, Happines Seneda, alisema mkoa umeendelea kutekeleza mkakati wa lishe kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali.

# Wafanyakazi 6,800 wawasilisha madai WCF

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAFANYAKAZI wa sekta mbalimbali wamewasilisha madai zaidi 6,800 katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), kati yake asilimia 95 yametokana na ajali huku asilimia sita zikisababisha vifo vya wafanyakazi hao.

Mkurugenzi wa Huduma za Tiba na Tathmini wa mfuko huo, Dk. Abdulsalam Omary, alisema hayo juzi wakati wa mafunzo ya uelimishaji wa tathmini za ulemavu uliotokana na ajali na magonjwa yatokanayo na kazi.

Mafunzo hayo ya siku tano yanashirikisha madaktari wa mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Morogoro na Pwani yanayofanyika mjini Morogoro. Alisema kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita walipokea madai hayo na kwamba asilimia tano ni magonjwa yaliyotokana na sehemu ya kazi.

Alisema kutokana na madai hayo mfuko huo ulifanikiwa kulipa fidia ya Sh. bilioni 27 ambazo ni fedha nyingi kulipwa kabla ya kuanzishwa kwa mfuko huo. Alisema miongoni mwa matatizo yanayowakumba wafanyakazi ni wale wanaofanyakazi katika viwanda na kuendesha mitambo yenye sauti iliyopitiliza, hivyo kuathiri masikio na kukosa usikivu pamoja na wafanyakazi waliokuwapo katika sekta ya afya ambao huathiriwa na kuambukizwa kwa magonjwa ikiwamo kifua kikuuu.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, alisema mfuko umeanza utoaji wa mafunzo ya tathmini za ulemavu uliotokana na ajali na magonjwa yatokanayo na kazi kwa madaktari kuanzia mwaka wa fedha 2015/16, na kwamba hadi sasa jumla ya madaktari 1,085 kutoka wilaya mbalimbali wameshapatiwa mafunzo hayo.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, aliahidi kuwachukulia hatua waajiri wote katika mkoa huo, wanaokwepa kuwasilisha michango WCF.



Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Jiji la Dar es Salaam, Suzan Mdesa, akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, katika viwanja vya Shule ya Msingi Kitunda, jijini humo juzi. Wengine ni Mkurugenzi wa ALARM Tanzania, John Wambura (kulia), Ofisa Elimu Kata Kitunda, Festo Mlimila (wa tatu kulia) na Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kitunda, Claudia Gabriel. PICHA: BEAUTY MWAKATOBE WA TUDARCo

## RC: Miradi iliyosimama Mkuranga itengewe fedha

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, ameiagiza Halmashauri ya Mkuranga kutenga fedha kwa ajili ya kumalizia miradi iliyosimama kwa muda mrefu, ili kuwapa manufaa wananchi.

Kunenge alitoa agizo hilo juzi alipokuwa katika kikao cha baraza maalumu la madiwani, ambapo pamoja na kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), alitoa maagizo hayo.

Katika hotuba yake iliyosomwa na Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, Kunenge alisema miradi ya maendeleo imekuwa na manufaa kwa wananchi kwa kuwaondolea vikwazo kwenye maeneo yao, hivyo ambayo haijakamilika ni vema nguvu zikaelekezwa huko.

Alisema halmashauri hiyo imeonyesha kuwa na upungufu wa miundombinu ya vyumba vya madarasa 1,262 kwa shule za msingi na sekondari, hivyo fedha zinatakiwa kuelekezwa huko kutatua tatizo hilo.

Kunenge aliagiza pia kuimarisha usimamizi na udhibiti wa makusanyo ya ndani kwa vyanzo vya ndani vilivyopo kwa kufunga CCTV camera kwenye vyanzo vikubwa ambavyo njia zake zinajulikana.

Alimwagiza mkurugenzi kuchukua hatua za kinidhamu kwa idara au kitengo kitakachokuwa na hoja nyingi za ukaguzi.

Katibu Tawala Mkoa wa Pwani, Mwanaasha Tumbo, aliwataka watendaji kuzingatia kila kitakachofanywa kufuata taratibu na miongozo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Mshamu Munde, aliahidi kusimamia maagizo yaliyotolewa na mkuu wa mkoa, huku akisema watakuwa waangalifu kwenye miradi na manunuzi ya dharura.

## NACONGO kuchagua viongozi mwezi ujao

**Na Mary Geofrey**

BARAZA la Taifa la Uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NACONGO), linatarajia kufanya uchaguzi wake mkuu unaotarajiwa kufanyika Julai 8, mwaka huu.

Uchaguzi huo umetangazwa baada ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, kuunda kamati ya mpito ya watu 10 kutoka katika mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), ya kitaifa na kimataifa kwa dhumuni la kusimamia.

Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Uchaguzi wa Baraza la NACONGO, Wakili Flaviana Charles, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu uchaguzi huo, alisema fomu zitaanza kuchukuliwa Juni 21 katika ofisi za Maendeleo ya Jamii wilaya katika wilaya 139 nchini.

Alisema mwisho wa kurudisha fomu ni Juni 24 katika ofisi hizo hizo na Juni 25 uchakataji wa fomu za wagombea wa baraza katika ofisi hizo na kazi hiyo itafanywa kamati ya taifa ya uchaguzi.

Wakili Flaviana alisema Juni 26 uchaguzi katika ngazi za wilaya utaanza na Juni 28 uchaguzi wa wajumbe wa Baraza katika ngazi ya mkoa.

Alisema Julai 5 hadi 8 utakuwa ni uchaguzi wa viongozi wa kitaifa wa baraza, kamati ndogo na wajumbe wa bodi ya uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali.

## TALIRI yaja na utafiti wa tija kwa wafugaji

**Na Mbaraka Kambona**

TAASISI ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), imesema imejipanga kuhakikisha inafanya utafiti wa kutosha ili matokeo yake yatumiwe na wafugaji moja kwa moja badala ya utafiti wa mambo ya sayansi tu.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mkuu wa TALIRI, Prof. Erick Komba, baada ya kumaliza kikao kazi cha kujadili mkataba wa utendaji kazi wa taasisi hiyo kilichofanyika jijini Dodoma juzi.

Alisema lengo la taasisi hiyo ni kufanya utafiti na kueneza teknolojia ya utafiti huo ili kuendelea kuboresha tasnia ya mifugo.

"Tumejikita katika kufanya utafiti wa malisho na mifugo ili kuwafanya wafugaji waweze kufuga kwa tija na kunufaika na mifugo yao," alisema Prof. Komba.

Aliongeza kuwa katika kipindi cha uongozi wake, atahakikisha utafiti wanazofanya zinaendelea kuwanufaisha wafugaji na taifa kwa ujumla.

Aidha, Prof. Komba aliwahimiza watendaji wa taasisi hiyo kufanyakazi kwa weledi, na kwa bidii ili waweze kuzalisha utafiti wa kutosha na kuusambaza kwa wafugaji waweze kuutumia na kujiongezea kipato.

"Tangu nimeteuliwa kuongoza taasisi hii nina miezi miwili sasa, lakini mipango yangu ni kuhakikisha ninashirikiana kikamilifu na watafiti wenzangu kufanya tafiti zitakazoleta matokeo yatakayowasaidia wafugaji kupata tija na sio utafiti kwa ajili ya sayansi tu," alifanua Prof. Komba.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya TALIRI, Prof. Sebastian Chenyambuga, alisema wajibu wa taasisi hiyo ni kufanya utafiti, hivyo aliwataka watumishi wahakikishe wanajipanga vizuri ili kazi zao ziwe na manufaa kwa wananchi hususan wafugaji.

# TAMISEMI yafunguka Msalala kuwa wilaya

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema Halmashauri ya Wilaya ya Msalala haijaanza mchakato wa kuomba kuwa wilaya kwa kadri ya matakwa ya sheria.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, David Silinde, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Msalala (CCM), Kassim Iddi.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua lini serikali itaipandisha Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kuwa wilaya kamili. Akijibu, Silinde alisema Wilaya ya Kahama ni moja kati ya wilaya tano zinazounda Mkoa wa Shinyanga na kwamba utaratibu wa kuanzisha mkoa na wilaya mpya umebainishwa kupitia Sheria ya Uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya.

"Kwa mujibu wa sheria hii, utaratibu wa kuanzisha wilaya mpya huanzia kwenye Serikali za Vijiji/Mitaa ili kupata ridhaa ya wananchi kisha hupelekwa kwenye Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri, Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) na Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), alisema.

Naibu Waziri huyo alibainisha kuwa hatua hiyo, maombi hayo huwasilishwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa ajili ya uhakiki na kujiridhisha na baadaye kuwasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili akiridhia atoe kibali cha kuanzishwa kwa wilaya husika.



Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, akijibu maswali ya papo kwa papo Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kilwa yaboreshewa miradi ya maji

SERIKALI imesema katika mwaka wa fedha 2021/22, itaendelea kuboresha huduma ya majisafi na salama na yenye kutosheleza katika Wilaya ya Kilwa kwa kutekeleza miradi mbalimbali.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Maryprisca Mahundi, aliyasema hayo bungeni jana wakati akijibu swali la Mbunge wa Kilwa Kaskazini (CCM), Francis Ndulane.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itawafikishia huduma ya maji wananchi wa kata za Kipatimu, Kibata, Chumo, Kandawale, Namayuni, Miguruwe, Njinjo, Mitole na Kinjimbi katika Jimbo la Kilwa Kaskazini ili kuwaondolea wananchi hao shida ya maji inayowakabili.

Akijibu, Naibu Waziri huyo alisema miradi ambayo itatekelezwa na kazi ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu sita katika vijiji vya Mitole Kata ya Mitole, Zinga Kibaoni Kata ya Miguruwe, Namayuni Kata ya Namayuni, Kisima - Mkika Kata ya Njinjo, Kibata Kata ya Kibata na Ruhatwe Kata ya Kikore.

Pia alisema ujenzi wa miradi mitano ya mitandao ya mabomba na matangi ya kuhifadhia maji katika vijiji vya Kinjimbi Kata ya Kinjimbi, Chapita Kata ya Mingumbi, Chumo Kata ya Chumo, Marendego Kata ya Somanga na Kipindimbi Kata ya Njinjo.

Alisema katika vijiji hivyo kutajengwa vituo 50 vya kuchotea maji na kwamba katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya maji kwa kutekeleza miradi Wilayani Kilwa ambayo imehusisha uchimbaji wa visima virefu nane.

"Kadhalika, ukarabati wa tangi la maji la lita 45,000 katika Kijiji cha Kipatimu, ukarabati wa mradi wa maji Mtubei Mpopera katika Kata ya Kandawale na ujenzi wa vituo 11 vya kuchotea maji, kukamilika kwa kazi hizo kumeboresha upatikanaji wa huduma ya maji kufikia asilimia 68.5," alisema.




Habari zote na Augusta Njoji

# Mkandarasi Uwanja wa Ndege Musoma ndani ya miezi 18

BUNGE limeelezwa kuwa serikali imekamilisha mchakato wa manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi atakayetekeleza mradi wa ukarabati wa upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Musoma ndani ya miezi 18.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi. Mwita Waitara, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini ukarabati wa upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Musoma utakamiliki.

Akijibu, Waitara alisema mkataba kati ya Serikali na Mkandarasi Beijing Construction Group Co. Ltd umesainiwa Desemba, 2020 na utekelezaji wa mradi huo utakamilika kwa kipindi cha miezi 18 baada ya kuanza hatua za utekelezaji.

Naibu Waziri huyo alisema hivi sasa serikali inajiandaa kumalizia awamu ya pili ya malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi huu ili kuruhusu mkandarasi kuanza hatua ya utekelezaji wa ujenzi.

"Hata hivyo, serikali imeshamkabidhi mkandarasi eneo la mradi, nimhakikishie mbunge kuwa Serikali ina nia ya dhati ya kukarabati na kupanua Kiwanja cha ndege cha Musoma na utekelezaji wake utakamilika baada ya miezi 18 ya utekelezaji," alisema.

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Bupe Mwakang'ata amehoji lini barabara ya kutoka Kibaoni-Kasansa-Muze-Ilemba- Kilyamatundu-Mlowo itajengwa kwa kiwango cha lami.


Akijibu, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Godfrey Kasekenya, alisema barabara ya Kibaoni hadi Mlowo ni barabara ya mkoa yenye jumla ya urefu wa kilomita 363 na inaunganisha mikoa ya Katavi, Rukwa na Songwe.

"Barabara hii inapita katika bonde la Ziwa Rukwa ambalo ni maarufu kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na uvuvi na hivyo kuwa kichocheo kikubwa cha kiuchumi katika mikoa ya Rukwa, Katavi na Songwe," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali ilianza mipango ya kuijenga kwa kuanza na ujenzi wa daraja la Momba ambalo lilikuwa kikwazo kikubwa cha mawasiliano kati ya mikoa hii mitatu ya Rukwa, Katavi na Songwe ambao umekamilika.

"Ili kukamilisha ujenzi wa barabara yote kwa kiwango cha lami kuanzia Kibaoni hadi Mlowo (km 363), Serikali ipo katika hatua ya awali ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambapo kazi inaendelea kwa sehemu ya Kibaoni – Majimoto (km 27) iliyopo mkoani Katavi na sehemu ya Muze – Kilyamatundu (km 141) iliyopo Mkoa wa Rukwa," alisema.

Aliongeza "Kwa upande wa mkoa wa Songwe, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa sehemu ya Mlowo-Kamsamba (km 130.1) imekamilika na serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami."




Ukurasa 13

Wakuu someni ujumbe wenu huu!

BUFE
IJUMAA JUNI 18, 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

EWURA RASMI OPERESHENI KUSAKA 'VISHOKA' WAUNGANISHAJI UMEME

# Usimamizi bora wa mapato waipatia Halmashauri Ilala Hati Safi miaka 5

**Na Yasmine Protace**

KATIKA mambo yanayotafsiri ufanisi wa utendaji katika halmashauri mbalimbali, iwe ya jiji, wilaya, mji au mji mdogo, kuna angalizo ya ripoti ya hesbau zake kutoka kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Hapo ndani yake kuna majumuisho ripoti kuu tatu; mbaya, wastani na nzuri, ambayo kiutendaji ni katika halmashauri anaipigania katika kusimamia na kutumia fedha zake.

Pia kuna sura ya pili kuhusu uhalisi uliopo kwenye matumizi ya fedha hizo. Kimsingi, katika mamlaka zote za halmashauri, kuna vyanzo mbalimbali vya mapato yake, vikiibuliwa kwa ajili ya kutekeleza maendeleo ya wananchi wake.

Mara zote, vyanzo hivyo visiposimamiwa vyema, daima maendeleo hayatapatikana na vivyo hivyo, sura hiyo katika mapato na kinyume chake, kama halmashauri zitasimamia kwa weledi vyanzo vyake vya mapato, maendeleo daima yataonekana.

Hivi karibuni Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji Dar es Salaam, lilijadili na kutoa mapendekezo ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2020, wakati huo ilikuwa Manispaa ya Ilala.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Jumanne Shauri, alitangazia taarifa ya CAG kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, kwamba iliyokuwa Halmashauri ya Manispaa Ilala na sasa Halmashauri ya Jiji Dar es Salaam, imepata hati safi.



Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, wakati huo, ambayo mwaka huu imepandishwa hadhi kuwa Jiji la Dar es Salaam, wakiwa kikaoni. **PICHA: MTANDAO**

Hiyo anasema ni kipindi kinachoishia Juni 30, mwaka jana, ukiwa mwaka wa tano mfululizo, akifafanua: "Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 uliokaguliwa, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala imepata Hati Safi na kufanya halmashauri yetu kuendelea kupata hati safi kwa miaka mitano mfululizo kuanzia 2015/2016, 2016/2017, 2017/2018, 2018/2019 na 2019/2020."

Anaongeza kwamba CAG ana jukumu la kukagua taarifa za mapato na matumizi ya fedha za umma na kutoa matokeo ya ukaguzi, pia mapendekezo kutokana na ukaguzi huo, kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa na menejimenti ya uongozi husika.

Anaongeza kuwa, Kikao cha Baraza la Madiwani kina jukumu wa kupokea taarifa, kuijadili kwa kina na kutoa mapendekezo yatakayowezesha kufunga hoja husika.

**MAPENDEKEZO KIKAONI**

Hivyo, anasema kikao cha Baraza la Madiwani kimependekeza kwamba hoja zisizofungwa, ishughulikiwe kwa kufuata hoja za CAG, katika namna ya kushughulikia mapendekezo hayo na hoja zilizobaki zifungwe.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ilala, Ubaya Chuma, anaipongeza Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kupata hati safi.

"Naipongeza sana Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwa ushirikiano uliokuwapo baina ya menejimenti pamoja na wawakilishi wetu madiwani wakiongozwa na Mstahiki Meya uendelee, udumishwe," anasema.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija, pia alijitokeza kupongeza Baraza la Madiwani na watendaji, kwa kupata hati safi.

"Nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Mstahiki Meya na madiwani wako lakini na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na wataalamu wako kwa kupata Hati Safi.

"Hii inaonyesha kwamba, fedha za serikali mnazozikusanya, hasa ikizingatiwa kwamba jiji la Dar es Salaam ndiyo inayoongoza kwa ukusanyaji mapato na tunavyoona kwamba mmepata hati safi, maana yake inatudhihirishia fedha mnazozipokea zinakwenda kutumika kama zilivyopangwa," anasema.

**RC MAKALA**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, anawaasa madiwani wawasimamia wataalamu waweze kuzimaliza hoja ambazo hazijafutwa.

Anataja sehemu ya majukumu yake Mkuu wa Mkoa, ni mamlaka za serikali za mitaa katika mambo ya fedha, pia kuzisimamia, kwa maana hiyo, ni kiongozi wa shughuli zote za serikali mkoa.

"Nyie ni mashahidi hata bajeti zenu anayewakilisha kwenye kamati ni Mkuu wa Mkoa, kwa hiyo hata dosari zozote zinapotokea anayenyooshewa kidole ni Mkuu wa Mkoa.

"Kwa hiyo, na mimi najenga imani kwenu, nilichokishuhudia, mlichokijadili ushauri uliotolewa na wataalamu kwa maana menejimenti, mkaguzi, maoni ya kamati ya fedha na ambayo mmeyapata Baraza la Madiwani, msiniangushe mkayatekeleze," anasema.

Anaziasa Halmashauri za Jiji, kupitia imani waliopata kupitia kwea madiwani, nao wanatakiwa kutekeleza walioshauriwa na CAG, yale maagizo ya Kamati ya Bunge.

"Kwa hiyo, sisi tunaondoka tukiamini kwamba maamuzi yaliyokwishafanyika ya kushughulikia hoja mbalimbali basi yatatekelezwa na nyie waheshimiwa madiwani, wasimamieni wataalamu waweze kutimiza hayo," anasema.

UCHUMI

# EWURA RASMI OPERESHENI KUSAKA ‘VISHOKA’ WAUNGANISHAJI UMEME

## • ‘Vigezo na masharti’ kumiliki leseni
## • Ikithibitika jela miaka 5, faini mil. 10



Mafundi umeme wa majumbani wakiwa kazini. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MAUDHUI ya Sheria ya Umeme ya Mwaka 2008, yanasema ufungaji nyanya za umeme, ni shughuli inayotakiwa kufanywa na mwenye leseni inayotolewa na Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Mojawapo ya jukumu la EWURA, ni kusimamia sekta ndogo ya umeme zinazojumuisha ufungaji wa umeme majumbani, viwandani na sehemu nyingine.

Hivi sasa sekta ya nishati inakabiliwa na wimbi la mafundi wababaishaji maarufu ‘vishoka’ ambao hawana leseni kutoka EWURA.

Katika kupambana na ‘vishoka’, Kaimu Mkurugenzi wa EWURA, Mhandisi Godfrey Chibulunje, anasema uunganishaji usiozingatia utaalamu husababisha madhara mbalimbali, ikiwamo nyumba kuungua au kupata hitilafu za umeme kila mara.

Anasema, hivi sasa EWURA imeandaa kanuni za kusimamia ufungaji wa mifumo ya umeme za mwaka 2019 ambazo zinatumika.

Chibulunje anasema, bado kuna tatizo la mafundi wengi wasiosajiliwa na wanafanya kazi bila ya usimamizi, hivyo kazi nyingi zinafanywa chini ya viwango na kusababisha ajali za moto muda mfupi baada ya kukamilika.

**WATAKAVYOWABANA**

Mhandisi Chibulunje anatahadharisha kwamba, yeyote anayefanya kazi ya umeme bila leseni ya EWURA, adhabu yake ni kifungo cha miaka mitano au faini isiyozidi Sh. milioni 10, au adhabu zote mbili.

“Sisi EWURA tunaendelea na mapambano dhidi ya mafundi wanaofanya kazi za kuunganisha mifumo ya umeme bila kuwa na leseni, utoaji wa leseni za uunganishaji unalenga kuweka utaratibu wa kisheria,” anasema.

Pia anabainisha hatua za kuwatambua mafundi umeme wenye vigezo vya leseni, itasaidia serikali kutimiza azma ya kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na umeme kwa usalama zaidi kwa kuhudumiwa na mafundi wenye vigezo.

Mhandisi Chibulunje anasema, kwa sasa wanalenga kukabiliana na wimbi la ‘vishoka’ wanaounganishia watu umeme kinyume cha sheria, hivyo kusababisha madhara makubwa kwa usalama wa watu na mali zao.

“Maombi ya leseni ya umeme hufanywa mtandaoni kupitia mfumo uitwao LOIS yaani ‘Licensing and Order Information System’ unaopatikana kupitia tovuti ya EWURA,” anasema.

Anaeleza kuwa, mwombaji anapaswa kuwa na nakala ya picha ya rangi ya bluu, wasifu, vyeti vya elimu ya ufungaji umeme, risiti ya malipo ya maombi ya leseni, hati ya kusafirisha au kitambulisho cha taifa na nakala za vyeti zilizothibitishwa.

“Baada ya kupokea maombi, EWURA huwasiliana na chuo alichosoma mwombaji ili kuthibitisha uhalali wa vyeti alivyowasilisha, baada ya kupata uthibitisho, maombi ya leseni huwasilishwa katika kamati ya leseni za umeme ili kupata mapendekezo ya daraja stahiki la mwombaji wa leseni,” anasema.

Anabainisha leseni za umeme zinatolewa katika madaraja mbalimbali kulingana na sifa za mwombaji.

“Daraja A ni fundi mwenye uwezo wa kufanya shughuli zote za ufungaji na usambazaji umeme, daraja B ni ufungaji umeme msongo wa kati hadi volti 33,000, daraja ‘C’ ufungaji umeme wa msongo usiozidi volti 400,” anasema.

Anaongeza: “Mengine ni daraja ‘D’ ufungaji umeme wa msongo usiozidi Volti 220, daraja ‘W’ atafanya kazi chini ya usimamizi wa mwenye leseni daraja A, B, C au D, S1 ni daraja la kazi maalum za umeme kwa misongo yote.”

Anafafanua S2 ni kazi maalum za umeme wa msongo hadi volti 33,000, S3 kazi maalum za umeme wa msongo hadi volti 1000.

Mhandisi Chibulunje anasema EWURA imejipanga kuhakikisha kazi ya uunganishaji umeme inafanywa bila ya kusababisha madhara ya kiuchumi, kijamii na kiafya.

Mkurugenzi huyo anasema, ili kukabiliana na mafundi wasio na leseni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linapaswa kuhakikisha linapokea kazi za mafundi waliosajiliwa na EWURA.

**KAULI YA WAZIRI**

Waziri wa Nishati, Dk.Medard Kalemani, anaiagiza TANESCO, kuhakikisha inapokea kazi za mafundi umeme waliosajiliwa na EWURA, ili kuleta nidhamu katika tasnia hiyo.

Akifungua hivi karibuni mafunzo kwa mafundi hao kuhusu sheria ya umeme na kanuni za ufungaji umeme iliyoandaliwa na EWURA, Dk. Kalemani anasema hatua hiyo itasaidia kupunguza athari za ajali zinazotokana na mifumo isiyo mizuri ya uunganishaji wa umeme kwa wateja.

“Naiagiza TANESCO kutumia kanzi data ya EWURA katika kupokea kazi za kandarasi za umeme na fundi yeyote mwenye leseni ya EWURA ana uhuru wa kufanya kazi popote Tanzania Bara,” anasema.

Kadhalika, anazitaka taasisi za serikali na watu binafsi kutumia mafundi ambao wamesajiliwa na wana leseni ili kuepukana na vishoka.

“Tatizo lililopo mafundi wengi wasiosajiliwa wanafanaya kazi bila usimamizi, wengine hawana leseni za EWURA na wengine wanatumia leseni mfu ambazo hawajazihuisha hadi leo,” akumbusha.

Pia anaitaka EWURA na taasisi zinazohusika kufanya uchambuzi wa bei halali za mafundi umeme majumbani, kuwa suala hilo kwa sasa halina kanuni, lakini kumekuwapo na utozaji bei kiholela na kuwa kero kwa wateja.

“Hawajui wanachokilipia ni nini ni (ufungaji waya) ‘wiring’? Au muhuri?, vijijini lugha inayotembea sana ni muhuri kwa hiyo analipia wiring na muhuri, kana kwamba hizo ni kazi mbili tofauti, kinachopaswa kulipiwa ni ufundi wako wa kumwekea nyaya mteja sio muhuri, muhuri unakutambulisha wewe,” anasema.

Waziri anasema kuanzia sasa mtu atakayefanya uunganishaji, umeme ndio anapaswa kugonga muhuri kwa kuwa unamtambulisha yeye na si kumlipisha mteja.

**RIPOTI KAZI**

Ripoti ya Utendaji Kazi ya Sekta Ndogo ya Umeme iliyotolewa na EWURA mwaka 2018/19, inaonyesha mamlaka hiyo ilitoa leseni 662 kati ya hizo 654 zilikuwa za ufungaji vifaa vya umeme na nane zilikuwa leseni za uzalishaji umeme.

Inataja kuwa mamlaka hiyo ilitoa leseni za usakinishaji (installations) wa umeme 654 na 600 katika mwaka wa fedha 2018/19 na 2017/18, ambazo zinaongezeka kwa asilimia 8.2.

Pia leseni 15 zilitolewa kwa wanawake na 639 kwa wanaume katika mwaka wa fedha 2018/19, wakati leseni 10 zilitolewa kwa wanawake na 590 kwa wanaume katika mwaka wa fedha 2017/18.

**KAULI YA WANANCHI**

John Richard, mkazi wa Dodoma, anasema sheria na kanuni zinazotungwa kwenye suala la uunganishaji umeme, zinapaswa kusimamiwa ili kujiepusha na madhara yanayotokana na kuunganishwa umeme chini ya viwango.

Anasema, mafundi wengi wasio na uwezo na elimu sahihi kuhusu vifaa vya umeme vinavyofaa, hujikuta wanaingia kwenye mtego wa kununua vifaa visivyokidhi viwango na kuishia katika majanga.




Israel Ilunde, Mkurugenzi wa asasi ya Vijana YPC, illiyo mstari wa mbele katika harakati za usindikaji.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Wakuu someni ujumbe wenu huu!






**NA JOSEPH KULANGWA**
+255 713 410008

TANGU nijue serikali ni nini, sijawahi kusikia duniani isiyo na mawaziri. Ila niliwahi na ninaendelea kuelimishwa kuwa mawaziri ni watu muhimu sana serikalini, katika kumsaidia Rais au Mkuu wa Nchi kutekeleza majukumu yake.

Ninaendelea kuamini hivyo, ndiyo sababu utasikia waziri yuko mahali akijinasibu kumwakilisha Rais. Utamsikia waziri bungeni akijibu maswali kwa niaba ya serikali, hiyo ujue ni kwa niaba ya Rais ambaye huhusika kwa asilimia 100 kumteua.

Hivyo, ukiteuliwa kuwa waziri, ujue Rais kakuamini kwa kiwango cha juu, kuwa hutamwangusha. Ujue Rais anataka utekeleze yale aliyoahidi wakati akizunguka huku na kule kutafuta kura kwa wananchi.

Maana yake ni kwamba, kama waziri hatafanya hivyo, anafanya raia wamuone hayuko sawa kwa wananchi waliomwamini, wakamwelewa katika ahadi zake na kumchagua kuwaongoza. Hapo ndipo sasa waziri anapokuwa amebeba roho ya Rais kisiasa.

Hata hivyo, kuna nyakati Rais hukosea katika uteuzi wake, ama kwa kuyumbishwa na wanaomshauri, au kwa kudhani kwake tu kuwa huyu nikimpa hiki atakiweza, lakini hatimaye huja tofauti na alivyotarajia.

Ilipokuwa inatokea hivyo, enzi za Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli alikuwa ‘akiwatumbua’ tu bila kuangalia makunyanzi na kila mara akiwaonya kuwa usifanye sherehe unapoteuliwa, kwa kuwa hujui utadumu hadi lini.

‘Aliwatumbua’ sana enzi zake. Watu hawakuishi kwa kubweteka, kwa kuwa nimekuwa waziri basi ni mpaka miaka 10 ijayo, mpaka niondoke naye madarakani. Dk. Magufuli hakuwa hivyo, unateuliwa asubuhi, jioni jua likizama hauko sawa unazama nalo.

Hii maana yake ni kwamba, lazima unapopewa jukumu na mtu anayekuamini lifanye kwa imani ile ile, kurudisha shukurani yako kwa aliyekuona unafaa. Ukishindwa unamfanya naye ashindwe, akikutazama usoni atakuonea haya, hivyo utakuwa umemwangusha.

Unajiuliza, kwanini leo nimeanza na haya? Ni kutokana na ninachokiona leo katika ‘nji’ hii. Naamini kabisa ‘nji’ ya Tanzania ina mawaziri wengi wazuri na wapo wapya na wakongwe, ambao piga ua kila uteuzi wamo, akija Rais mpya wamo.

Sijamwona anayeharibu kazi yake mpaka kustahili kung’olewa na Mama Samia, lakini yawezekana kuna baadhi wanafanya kimazoea tu, kuwa nitaletewa taarifa, nitaagiza, litatekelezwa, bila hata kunyanyua mguu kwenda eneo la tukio kujiridhisha.

Nchi hii inaundwa na vijana na wazee, wanawake na wanaume, watoto na wakubwa. Lakini, katika nchi hii wazee wanateseka sana. Sijui ni kwa kuwa wamezeeka, hawawezi tena kutoa sauti, pengine hata wakitoa sauti haisikiki! Unajua tena uzee.

Jenista Mhagama, ni mmoja wa mawaziri waandamizi katika serikali hii. Amepewa jukumu kubwa la kushughulika na kazi na ajira. Kwa kuwa wizara zetu hizi ni mtambuka, wazee wanashughulikiwa na Dada Doro, lakini wanapokuwa kazini wanashughulikiwa na Dada Jeni. Wanapodai mafao yao wanakuwa chini ya Dada Jeni.

Hivi Dada Jeni anajua kinachofanyika katika mifuko ya hifadhi ya jamii ambako wazee wastaafu wana michango yao? Anajua kuwa kuna mashirika na kampuni za umma na binafsi hazijapeleka michango kwa miaka sasa?

Anajua wazee kila kukicha ni mguu na njia kufuatilia mpaka wengine wanakata tamaa kama si kufariki dunia bila kulipwa? Ameshahakiki ni mashirika, kampuni au taasisi ngapi hazijapeleka na hazipeleki michango ingawa zinakata? Anatembelea huko kwenye maeneo ya matukio?

Dada Jeni, anajua ni vipi wazee waliofanyiwa ukatili makazini na kwenda kulalamika kwenye Tume za Usuluhishi wanavyoswagwa na kuzungushwa, kisa bado ni kitendawili? Kesi zinaahirishwa mpaka wanakata tamaa kama si kufariki dunia?

Dada Jeni anajua ni kivipi mashirika, kampuni na taasisi za umma na zisizo za umma suala la ajira kuna mtihani ndani yake. Mawaziri tokeni bungeni na ofisini, muwende mkajionee, mumsaidie Rais Samia, Kazi lendelee! Ohooo! Alamsiki!

BIASHARA

PPP AWAMU INAYOKUJA...

# Miradi ya ubia iepushe ya IPTL, City Water na Rites

- Mipya iko 41, thamani yake trilioni 3/-
- Serikali: Sera, sheria zimezuia 'upigaji'

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Tanzania inajiandaa kutekeleza miradi mipya 41 ya maendeleo, yenye thamani ya Sh. trilioni 3.02 kupitia ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), kuna dalili za nchi kupaa kimaendeleo.

Kimsingi PPP nchini ilianza katika sura ya sera na mkakati, lakini baadaye ikatungiwa sheria rasmi ya kuisimamia na ndio imekuwa mwongozo wake mkuu kwa sasa.

Utekelezaji wa miradi hiyo, ni sehemu ya Mpango Mkakati wa Taifa wa miaka mitano, unaoelezwa kwamba utaiwezesha nchi kutekeleza miradi ya ubia kwa ufanisi, ikiwamo kutengeneza ajira zaidi, kuongeza utaalamu, ubunifu, uzoefu na teknolojia.

Kadhalika, kasoro zilizojitokeza katika miaka ya nyuma na kuisababishia nchi hasara ilipokuwa inakodisha mashirika ya umma kwa wawekezaji zitaepukwa.

**KATIBU MKUU FEDHA**

Emmanuel Tutuba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, amebainisha hayo hivi karibuni jijini Arusha, kwenye warsha ya kuwajengea uelewa wahariri wa vyombo vya habari kuhusu ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi, iliyoandaliwa na Idara ya PPP iliyoko chini ya wizara hiyo.

Tutuba anasema: "Kufikia Mei 31, mwaka huu (siku 18 zilizopita) kulikuwapo na maandiko ya miradi 41 yaliyoandaliwa chini ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi. Hii inahusisha Maji, Afya, Elimu, Miundombinu, Mawasiliano, Ujenzi na Biashara."

Tutuba, ambaye kwa mamlaka ndiye mlipaji mkuu wa serikali, anaongeza kwamba miradi 40 kati ya hiyo imeibuliwa na mamlaka mbalimbali za serikali, wakati sekta binafsi imekuja na mradi mmoja.

Anaweka wazi msimamo wa serikali katika kutambua mchango muhimu wa sekta binafsi katika kusaidia kusukuma gurudumu la maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kupitia ubia katika uwekezaji mkubwa.

Kwa mujibu wa Tutuba, Tanzania inahitaji kutumia fursa zilizopo kuwavutia mitaji inayoongezeka ya sekta binafsi ambayo ni muhimu katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo Mwaka 2025 na Mkakati wa Taifa wa Kukua na Kupunguza Umaskini (NSGRP).



Emmanuel Tutuba, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango. **PICHA: MTANDAO**

Anafafanua kwamba, utaratibu wa PPP kwa Tanzania pia ni silaha muhimu ambayo katika kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi, na pia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi na umekuwa ukitambulika kama njia endelevu katika kutatua vikwazo katika kugharamia, kusimamia na huiendeleza mali na huduma za serikali pamoja na kushirikisha sekta zote katika ujenzi wa taifa.

Namna ubia kati ya sekta ya umma na binafsi unahusisha makubaliano ya pamoja, ambayo sekta binafsi hujihusisha na shughuli za ukarabati, ujenzi, uendeshaji, uendelezaji na kuendesha miradi kwa ujumla au baadhi ya maeneo, lakini kukizingatia kuwapo matokeo mazuri yanayolengwa.

Ushiriki katika miradi ya ubia unahusisha sekta ya uzalishaji au huduma za kijamii na kiuchumi kama vile kilimo, miundombinu, uzalishaji wa bidhaa, elimu, afya, utalii, nishati, maji, uendelezaji ardhi na mazingira.

Miradi hiyo, pia inahusisha ulinzi wa miundombinu, michezo, mawasiliano, teknolojia ya habari na mawasiliano, biashara, burudani na kilimo, pamoja na umwagiliaji.

Tutuba anasema licha ya dhana ya PPP sio ngeni kwa Tanzania kwani kabla ya kutungwa kwa sera ya PPP mwaka 2009, serikali ilihusisha sekta binafsi kutekeleza baadhi ya miradi ya IPTL, City Water na Rites-India.

Hata hivyo, miradi hiyo...haikufanikiwa kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa mazingira wezeshi yenye kuelekeza taratibu za kufuata katika kufanya maandalizi kabla ya kuingia kwenye mikataba ya PPP kwa lengo la kuleta tija na manufaa kwa taifa.

**NINI MWAROBAINI?**

Tutuba anadokeza kwamba kutokana na hali hiyo, hatua zilichukuliwa kudhibiti taifa kupata hasara kwenye miradi hiyo, kwa kuandaa Sera ya PPP pamoja na sheria yake ili kuwa na utaratibu mzuri wa kushirikisha sekta binafsi kwa kutumia nyenzo hiyo ya PPP.

Hali kadhalika, serikali nayo kupitia Wizara ya Fedha na Mipango inahakikisha miradi iliyopangwa kutekelezwa kupitia programu ya PPP, inafanyiwa uchambuzi wa kina na timu za wataalamu zinazoundwa kutoka taasisi mbalimbali za serikali.

Kamishna wa PPP, Dk. John Mboya, anasema wadau kutoka sekta binafsi wanakaribishwa, kwa kuwa taratibu za serikali zimeanzishwa kutokana na uamuzi wa serikali wa kuboresha na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi.

"Moja ya mipango ya serikali ni utekelezaji wa uamuzi ni kuandaliwa kwa Sera ya PPP ya mwaka 2008, Sheria ya PPP ya mwaka 2009 Sura 103 na Kanuni zake," anasema Dk. Mboya.

Kwa mujibu wa Dk. Mboya, utekelezaji wa miradi kwa ubia utainufaisha nchi na wawekezaji wabia, serikali ikipata kodi, wananchi wananufaika kwa kupata ajira na baada ya muda wa mradi kukamilika utabaki serikalini, wakati mwekezaji mbia atatengeneza faida kwa kuendesha mradi.

Dk. Mboya anaeleza kwamba, ni jitihada zitakazochangia ujenzi wa uchumi wenye ushindani, ukiwamo wa viwanda kwa maendeleo ya watu, ili ifikapo mwaka 2025/26 serikali ipate utaalamu, ubunifu na teknolojia kutoka sekta binafsi.

Katika kuhakikisha kwamba umma na wadau wanaielewa dhana ya PPP, Dk. Mboya anasema wameanza kutoa elimu na kwamba wameshawafikia watu zaidi ya 800 na wanaendelea na mchakato huo. Miongoni mwa walengwa ni halmashauri ambazo pia zitatekeleza miradi ya PPP.

Anasema, awali halmashauri zilikuwa na mtazamo hasi kuhusu utekelezaji wa miradi ya ubia, lakini kwa sasa mtazamo huo umekuwa chanya.

Kamishna Msaidizi wa PPP, Bashiru Taratibu, anawaondolea wasiwasi wanaohofia kuwa utekelezaji wa miradi mikubwa chini ya utaratibu wa PPP utaiingiza serikali katika hasara kama ilivyotokea miaka ya nyuma.

Anasema kwamba sera, sheria na kanuni za PPP zimetengenezwa vizuri, kiasi kwamba hakutakuwa na mianya hiyo, akiwa na ufafanuzi: "Kwa jinsi zilivyoandaliwa, serikali haitaingia tena kwenye mkenge."

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo, waliitahadharisha serikali kutorudia makosa wakati wa utekelezaji miradi ya PPP kutokana na kasoro zilizojitokeza katika miradi iliyopita kama ya umeme wa IPTL; reli uitwao Rites-India; na City Water kwenye maji.

Kadhalika, waliahidi kuwa vyombo vya habari vitaendelea kushirikiana na serikali kueleza umma kuhusiana na miradi inayotekelezwa kupitia PPP, ili wananchi wafahamu kazi kubwa inayofanywa kwa maendeleo ya taifa.

Mshiriki Beny Mwang'onda, alisema dhana ya PPP bado ni geni kwa Watanzania na kwa wananchi wengi, hivyo aliishukuru wizara kuandaa mafunzo hayo, ambayo alisema yamewapa uelewa wa kuelimisha umma.

"Jukumu letu ni kuhabarisha umma na tutafanya hivyo kuhakikisha wananchi wanakuwa na uelewa wa PPP, na namna unavyoweza kuleta matokeo chanya kupitia uwekezaji unaofanywa na sekta binafsi," Selina Mathew.



# Uzalishaji kahawa wazidi kudorora

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MWENENDO wa uzalishaji wa kahawa nchini bado ni mdogo licha ya Tanzania kuwa na fursa ya ardhi kubwa kwa nchi za Afrika Mashariki, imeelezwa.

Kutokana na hali hiyo, serikali imewataka wadau wa zao hilo kutoa mapendekezo ya kuboresha ili kuongeza ufanisi kwenye uzalishaji wake.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kongamano la 11 la wadau wa kahawa kwa mwaka 2021.

Alisema uzalishaji wa kahawa mwenendo wake si mkubwa sana huku akitolea mfano wa mwaka juzi kuwa ulikuwa tani 68,000 wakati Uganda ulikuwa tani 400,000.

"Naamini kupitia kongamano hili, tutajadili kwa pamoja ili tuondokane na uzalishaji mdogo. Hata kule kwangu Songwe uzalishaji unashuka tofauti na ilivyokuwa awali. Wakulima wanahama kwenye uzalishaji, hivyo kupitia kongamano hili tutajua sababu ili tuje na mikakati ambayo itajibu maswali juu ya tatizo hili," alisema.

Alitaja kero zingine zinazokabili sekta hiyo ndogo kuwa ni tija, uzalishaji mdogo, kuyumba kwa bei, ukosefu wa mitaji kwa wakulima na kutokopesheka kwenye taasisi za fedha, hivyo kuwafanya watu kuamini kuwa kilimo hakilipi.

Mgumba aliwataka wadau wa kahawa kutumia fursa hiyo kusikiliza kwa makini mawasilisho yatakayotolewa kwenye kongamano hilo na kutoa mapendekezo ya kuboresha zao hilo.

"Kahawa ni moja ya mazao ya kimkakati ambayo yanatakiwa kubadilika na kukua na kutoa mchango wa serikali kwenye tatizo la ajira, kukuza uchumi na kuongeza kipato kwa wakulima," alisema.

Mgumba alisema wadau hao wana jukumu kubwa la kuhakikisha lengo la serikali linafikiwa na uzalishaji kahawa unabadilika kwa kuongeza ufanisi.

"Tuje na mbinu na mipango mipya itakayotoa ufumbuzi wa changamoto kuu zinazokabili zao la kahawa ikiwamo udumavu kwa uzalishaji wa kahawa," alisema.

Mgumba alisisitiza kwamba sekta binafsi ndiyo injini ya uchumi na kwamba serikali itaendelea kutoa kipaumbele kwa sekta hiyo ili kufikia mapinduzi kwenye kilimo.

"Serikali imedhamiria kuleta mapinduzi kwenye kilimo na hatuwezi kusema tunaenda kwenye mapinduzi ya kilimo cha biashara bila sekta binafsi," alisema.

Aliwahakikishia wadau kuwa serikali itaendelea kushirikiana na sekta hiyo ili kufikia mageuzi kwenye kilimo huku akisema serikali itaendelea kuendeleza kilimo cha mkataba ili kulinda wawekezaji mitaji yao kwenye kilimo.

"Sekta binafsi tunawaona mara nyingi kwenye uzalishaji, serikali awamu ya sita itaheshimu kilimo hicho ili kuwavutia wawekezaji na si kuwachukulia kama madalali, kilimo kinahitaji fedha sasa yule anayewekeza ndio umdharau serikali ya awamu ya sita imesema haiwezi kufanya hilo," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Kahawa Tanzania, Prof. Aurelia Kamuzora, alisema kongamano hilo watajadili sababu za baadhi ya wakulima wa kahawa kukimbilia kuuza Uganda ili kushauri serikali kuondoa vikwazo na kuleta tija kwenye uzalishaji wa zao hilo.



Mkazi wa Kitongoji cha Chukuyu B, Kata ya Buigiri, wilayani Chamwino, Jackson Masinga (kulia), akitoa malalamiko yake kwa viongozi wa ngazi ya wilaya, kata na kijiji (waliokaa kushoto), jana, kuhusu halmashauri ya wilaya hiyo, kushindwa kulipa fidia kwa wananchi wapatao 119 wa kitongoji hicho, ambao wamezuiliwa kufanya shughuli zozote za ujenzi na kilimo kwa kipindi cha miaka 10 sasa. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mkakati waja kuunganisha kilimo na wadau

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo inatarajia kuandaa mpango mkakati wa kuziunganisha shughuli za wadau wa maendeleo kutoka balozi na mashirika ya kimataifa wanaofanya miradi ya maendeleo nchini.

Akizungumza juzi jijini hapa, Waziri wa Kilimo, Prof. Aldof Mkenda, alisema lengo ni kukuza sekta ya kilimo ili iwe na tija kwenye utafiti, kuzalisha mbegu za kutosha na huduma za ugani.

Prof. Mkenda alisema kipaumbele kingine ni katika suala la umwagiliaji, utafutaji masoko namna ya kupata fedha kwa ajili ya kuendesha kilimo.

"Nimetumia muda mrefu sana kuwaeleza ili kuhakikisha kwamba nguvu zote zinazoingia katika kilimo zinaelekea upande mmoja wa kuleta matokeo chanya," alisema Prof. Mkenda.

Hata hivyo, alisema kwa sasa kuna juhudi nyingi ambazo zinaendelea nchini lakini wizara inakuwa haina taarifa nazo.

"Utasikia kuna ubalozi fulani unafanya jambo Singida, Marekani wako Arusha au Canada wapo Dodoma, hivyo wizara inahitaji kujua watu hao wanafanya shughuli gani ili kuunganishwa.

"Tunataka kuwashawishi hawa ili wote tuelekee upande mmoja ambao tunahitaji kwenda nao," alisema Prof. Mkenda.

Alibainisha kuwa wizara imeanza na huduma za ugani kwenye mikoa ya Dodoma, Singida na Simiyu kwa ajili ya uzalishaji wa alizeti.

"Kwenye uzalishaji wa alizeti nchini tumejadili namna ya upatikanaji wa mbegu bora na jinsi ya kuwaunganisha wakulima kwa teknolojia ili na wenyewe waingie katika juhudi za serikali," alisema. Kadhalika, alisema tayari ameshazungumza na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) ili waunganishe nguvu kujua wako sehemu gani ili kufanya kitu ambacho kitasaidia kuleta matokeo chanya.

"Tumelenga kufanya hivi kwa sababu suala hili ni muhimu sana, kwa sababu bila wakulima hakuna kilimo," alisema.

Naye Naibu Mkurugenzi wa Ofisi ya Ukuzaji Uchumi katika Shirika la Kimataifa la Misaada la Marekeni (USAID), Andrew Read, alisema wanakubaliana namna sekta ya kilimo inavyofanya nchini, hivyo wako tayari kushirikiana ili kuwa na ufanisi.

# Kanisa lahamasisha uchangiaji wa damu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KANISA la Mlima wa Bwana jijini Dodoma, limehamasisha waumini wake kushiriki katika ibada maalum ya uchangiaji wa damu ili kuokoa maisha ya wagonjwa.

Hatua hiyo inatokana na kubainika kuwa uhaba wa damu katika hospitali, vituo vya afya na zahanati nchini unaelezwa kuwa moja ya sababu kubwa za vifo vya wajawazito, watoto na majeruhi wa ajali.

Askofu Mkuu wa kanisa hilo, Silvanus Komba, alisema jana kuwa kutokana na hospitali nyingi nchini kukabiliwa na uhaba wa damu, wameona kuna haja kwa kanisa kuchangia damu itayokwenda kusaidia wahitaji.

"Tunatambua kuwa kazi kubwa ya kanisa au viongozi wa kanisa ni kuwahudumia watu kimwili na kiroho pamoja na kuwafariji, kuwatia moyo waliokata tamaa ili kusonga mbele.

"Pamoja na hiyo, Kanisa la Mlima wa Bwana linatambua kuwa kuna mahitaji mengi ya damu kutokana na kuwapo kwa ajali, wajawazito pamoja na watoto. Kutokana na hali hiyo, kanisa limeona lifanye ibada pamoja na uchangiaji damu," alisema Askofu Komba.

Aliwataka Watanzania kutambua kuwa ni jukumu la kila mtu mwenye vigezo vya kuchangia damu kujitolea damu kwa lengo la kuwasaidia wahitaji badala ya kusubiri kutoa damu pale tu anapokuwa na matatizo.

Mmoja wa waumini wa kanisa hilo aliyechangia damu, Iren Ngongi, alisema kuwa kitendo cha kanisa hilo kuchangia damu ni sadaka kubwa ambayo wameitoa kwa watu wenye uhitaji.

"Leo kanisa limepata fursa ya kuchangia damu, damu inayochangiwa leo huwezi kujua itamsaidia nani kitendo hiki cha kuchangia damu kinaonyesha upendo, mshikamano na nitowe wito kwa Watanzania kuwa na moyo wa kujitolea damu ili kuokoa maisha ya watu," alisema.

Naye Mtaalamu kutoka kituo cha Damu Salama Dodoma, Charles Ndahani, alisema pamoja na juhudi za ukusanyaji wa damu bado kuna uhitaji mkubwa wa katika maeneo mengi.

Alisema damu inayokusanywa na kuhifadhiwa katika benki ya damu ni kwa ajili ya kuwapatia wahitaji na haiuzwi kama ambavyo baadhi ya watu wanadai.



# Watoto 900 wafanyiwa ukatili wa kijinsia

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

ZAIDI ya watoto 900 katika kipindi cha mwaka 2019/2020 mkoani Mbeya wamefanyiwa ukatili wa aina mbalimbali ikiwamo wa kingono, kutelekezwa na kunyimwa haki ya kupata elimu.

Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Dk. Angelina Lutambi, aliyasema hayo juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo yalifanyika kimkoa katika kijiji cha Ipinda, wilayani Kyela.

Alisema watoto waliofanyiwa ukatili huo ni kuanzia miaka sifuri hadi 14 na watoto 196 walifanyiwa ukatili wa kingono, wa kimwili 222, kihisia 296 na kutelekezwa 84.

"Takwimu hizi ndugu zangu ni mbaya, zinaonyesha ni jinsi gani jamii haiwajibiki na haijazingatia sheria katika kuwajibika kumlinda mtoto na vitendo vya unyanyasaji wa watoto huanzia ngazi ya familia, yatupasa kubadilika na kuongeza umakini katika malezi ya watoto na kudumisha amani na upendo ili kuepusha madhara kwa watoto," alisema Dk. Lutambi.

Alisema madhara yanayoweza kujitokeza endapo wazazi hawatakuwa na malezi bora kwa watoto ni kuwa na idadi kubwa ya watoto yatima, wanaoishi katika mazingira magumu ambao wengi wao huishia kuwa ombaomba mitaani na kujiingiza kwenye vitendo vya uhalifu, pamoja na kuongezeka kwa maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Alisema vitendo hivyo vinakwenda kinyume na tamko la kimataifa la 1990, Sera ya maendeleo ya mtoto pamoja na sheria ya mtoto ya mwaka 2009 kifungu namba 21 hivyo ni jukumu la kila mmoja kuweka mikakati ya kuhakikisha wanapata haki zote za msingi kwa ajili ya maendeleo na ustawi wao.

Katika kukabiliana na ukatili kwa watoto mkoani Mbeya, Shirika la Walteread limeanzisha programu mbalimbali ikiwamo mradi wa dream wenye lengo la kuwawezesha watoto kiuchumi na kupinga ukatili dhidi yao.

Mwakilishi wa Shirika la Walteread, Emmanuel Bahemana, tumeendelea kutoa elimu ya kujikinga na mazingira hatarishi ikiwamo kujikinga na maambukizi ya virusi vya Ukimwi kwa makundi hatarishi, elimu ya mabadiliko ya dunia.

Hata hivyo, Jukwaa la Watoto mkoani Mbeya limeipongeza serikali kwa kutunga Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 ambayo imedai imekuwa nguzo imara katika kudai na kutetea haki za watoto nchini.

Mwenyekiti wa Jukwaa hilo mkoani Mbeya, Eva Mwasongwe, ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Sekondari ya Ikama, wilayani Kyela, alisema sheria ya mtoto imewapa nguvu ya kupigania haki zao.

Alisema kupitia sheria hiyo wadau na mashirika mbalimbali wamewekeza nguvu kwao ili kuhakikisha wanapata haki zao za msingi pamoja na kukabiliana na vikwazo vinavyowakabili ikiwamo, ukatili wa kijinsia.

Aliiomba serikali kuendelea kusimamia na kuboresha sheria mbalimbali ambazo zimepitwa na wakati ili kumlinda mtoto na kutimiza haki yake.



Mkuu wa Wilaya ya Ileje, mkoani Songwe, Joseph Mkude, akivuna mahindi katika moja ya mashamba ya wakulima wa Kata ya Mbebe juzi, ikiwa ni wiki ya uvunaji inayosimamiwa na kampuni ya Ekari Moja ambayo inawasaidia wakulima elimu ya kilimo bora na kuwakopesha pembejeo za kilimo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Maofisa watendaji wapewa jukumu kufuatilia wajawazito

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAOFISA watendaji wa vijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wametakiwa kufuatilia na kuweka utaratibu ambao utawezesha wanawake wote wanaopata ujauzito wanakwenda kujifungulia kwenye vituo vya afya ili kuepusha hatari wanayoweza kuipata wanaojifungulia majumbani, ikiwamo vifo visivyokuwa vya lazima.

Maagizo hayo, yalitolewa jana na Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Dk. Leonard Msuya, wakati akipokea miradi mitatu ya vyoo vilivyojengwa kwenye vituo vya afya na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) kupitia mradi wa SAWA.

"Watendaji wote wanajukumu la kuwatambua wajawazito katika maeneo yao, msiwaachie wahudumu wa afya peke yao kwa sababu ni wachache hawataweza kufika katika kila eneo, hakikisheni mnatoa elimu juu ya lishe na mambo mengine ambayo yanahitajika kuimarisha afya za wajawazito," alisema Dk. Msuya.

Akikabadhi miradi hiyo Mwakilishi wa mradi wa SAWA, Mhandisi Upendo Judica, alisema kiasi cha Sh. milioni 192 kimetumika kukamilisha miradi hiyo.

Alisema katika vituo vitatu vya afya jumla ya matundu 21 ya vyoo vimejengwa na sehemu za kujifungulia kinamama pamoja na ujenzi wa miundombinu rafiki wa watu wenye ulemavu katika maeneo hayo ya kutolea huduma za afya.

Wananchi wa Kijiji cha Ilindi, waliishukuru Shirika la UNICEF kwa msaada huo ya matundu ya vyoo, jengo la kujifungulia kina mama na miundombinu kwa watu wenye ulemavu na kwamba wataendelea kutunza miundombinu hiyo kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

Flora Mwanjuguja, alisema kinamama walikuwa wanapata tabu ya kukosa eneo la kujifungua hali iliyokuwa inawalazimu kutumia umbali mrefu kufuata huduma hiyo na kwamba baada ya UNICEF kuwapatia jengo la kujifungulia sasa wataendelea kubeba mimba.

# H'shauri yakopesha vikundi vya ujasiriamali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya Sh. milioni 460 ambazo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ilivikopesha vikundi vya wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu hazijarejeshwa kwa zaidi ya miaka mitatu huku sababu zikitajwa kuwa ni ukaidi wa vikundi hivyo.

Hali hiyo imesababisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, kuagiza halmashauri hiyo kuvipeleka mahakamani vikundi 35 vinavyodaiwa fedha hizo ili virejeshe huku akitaka busara zitumike kwa vikundi vya watu wenye ulemavu.

Akizungumza kwenye kikao maalumu cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo cha kujadili Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo, Zena Kapama, alisema vikundi hivyo vimekuwa vikisuasua kurejesha.

Alisema vikundi ambavyo vimekuwa vikisuasua zaidi kurejesha mikopo hiyo ni vya vijana na watu wenye ulemavu huku akidai kuwa wenye ulemavu wamekuwa wakisingizia kuwa hawana uwezo wa kurejesha kwa sababu ya hali zao.

"Lakini kwa mwaka jana vikundi vingi vilivyokopa fedha hizi viliamini kwamba pengine fedha hizi zilikuwa za bure kwa sababu ya uchaguzi mkuu kitu ambacho hakikua sahihi, lakini tatizo kubwa lipo kwa vikundi vya wenye ulemavu ambavyo havilipi kabisa," alisema Zena.

Alisema wamechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha vikundi hivyo vinarejesha fedha hizo ikiwamo kuvipeleka kwenye Serikali za Mitaa ili vishinikizwe kulipa, lakini ikashindikana na baadhi walivipeleka kwenye mabaraza ya kata.

Baada ya maelezo hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera aliagiza Idara ya Maendeleo ya Jamii kuanza kutumia nguvu kudai fedha hizo ikiwamo kuvipeleka vikundi hivyo mahakamani.

Alimtaka Ofisa Maendeleo ya Jamii kuorodhesha vikundi vyote ambavyo vinadaiwa fedha hizo na kuwasilisha orodha hiyo kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi (OCD) wa wilaya hiyo ili waanze kushughulikiwa huku akiitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kushirikiana na polisi kuwahoji.

"Nakupa muda mpaka Septemba 10, mwaka huu, uwe umefuatilia na kuhakikisha watu hawa wote wamerejesha fedha hizi haiwezekani fedha zote hizi ziwe nje na muda huo ukifika hujatekeleza hilo utalala ndani na utatupisha kwenye nafasi hiyo," alisema Homera.

Katika hatua nyingine Homera aliwapongeza watendaji wa halmashauri hiyo kwa kukusanya vizuri mapato na kuwa inayoongoza mkoani humo kwa kufikia asilimia 98 pamoja na utoaji wa mikopo kwa vikundi vya halmashauri.

Vile vile, aliipongeza halmashauri hiyo kwa kufikia asilimia 97 za usuluhishi wa kwenye mfumo pamoja na kufanya vizuri kwenye upandishaji madaraja ya watumishi.

Kwa mujibu wa sheria kila halmashauri nchini inatakiwa kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuendeleza shughuli zao.



# Rais Mwinyi aipongeza Ujerumani kuendeleza miradi ya maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameipongeza Serikali ya Ujerumani kwa utayari wake wa kuendelea kuiunga mkono Zanzibar katika kuendeleza miradi ya maendeleo.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi Ikulu, jijini Zanzibar wakati alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Regine Hess.

Katika mazungumzo hayo, Rais Dk. Mwinyi alimweleza Balozi Hess kuwa azma ya Serikali ya Ujerumani ya kuendelea kuisaida Zanzibar katika kuendeleza miradi ya maendeleo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuyafikia malengo yaliyowekwa.

Alisema kuwa serikali anayoiongoza pia, inathamini ushirikiano uliopo kati yake na Serikali ya Ujerumani na hatua yake ya kuendelea kuiunga mkono Zanzibar katika sekta ya afya ambayo itaendelea kuleta manufaa kwa wananchi wa Zanzibar. Alisema azma ya Serikali ya Ujerumani ya kusaidia uendelezaji wa mradi wa majisafi na salama pamoja na mitaro ya majitaka katika eneo la Mji Mkongwe itasaidia kuuweka mji huo katika hadhi yake inayohitajika na kuwasaidia wananchi kupata huduma hizo ipasavyo.

Alisema kuwa Serikali ya Ujerumani kwa muda mrefu imeisaidia Zanzibar kuimarisha na kuendeleza sekta ya afya ikiwa ni pamoja na kuzisaidia Hospitali ya Abdalla Mzee Pemba na Hospitali ya Kijeshi ya Bububu.

Rais Dk. Mwinyi alisema pamoja na Zanzibar kusaidiwa kuendeleza miradi katika sekta ya afya ni vyema ikasaidiwa uendelezaji miundombinu na mifumo ya afya pamoja na uendelezaji wa rasilimali watu ili kuwe na tija endelevu ya misaada inayotolewa.

Aliwakaribisha wawekezaji kutoka Ujerumani kuwekeza Zanzibar kwa kutumia fursa zilizopo hasa kupitia sera yake ya uchumi wa bluu, ndani yake kuna mambo mengi ya kuwekeza yakiwamo utalii, uvuvi, mafuta na gesi pamoja na kuzitumia rasilimali za bahari.

Alisema kuna haja kwa Serikali ya Ujerumani kuiunga mkono Zanzibar katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Covid-19 ambayo umeikumba dunia nzima.

Naye Balozi wa Ujerumani nchini, Regine Hess, alisema Zanzibar na Ujerumani zina historia kubwa ya ushirikiano na kwamba Ujerumani itaendeleza ushirikiano huo kwa kuiunga mkono serikali katika kuendeleza miradi iliyojiwekea.

Balozi Hess, alisema Serikali ya Ujerumani iko tayari kuiunga mkono Serikali ya Zanzibar kuimarisha miradi ya maendeleo ikiwamo huduma za majisafi na salama pamoja na mitaro ya majitaka katika Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Balozi Hess, alisema kwa upande wa Sekta ya Afya, Serikali ya Ujerumari iko tayari kuendelea kuiunga mkono Zanzibar kuimarisha sekta hiyo. "Juhudi za makusudi zitachukuliwa na Ubalozi wa Ujerumani katika kuitangaza Zanzibar kiutalii ikiwa ni pamoja na kuwaleta wawekezaji kutoka Ujerumani kuja kuwekeza hapa Zanzibar," alisema.

Balozi Hess alimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa juhudi zake alizozichukua za kuhakikisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa inaimarika na kuleta manufaa kwa nchi na wananchi wa Zanzibar.




Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Taifa, Yunus Ali Juma, akiwahutubia watoto, vijana na wazee katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yaliyoandaliwa na Baraza la Vijana Wilaya ya Magharibi A, Unguja juzi. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

## KMKM kuanza kujitegemea kwa kuwekeza miradi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), Commodore Azana Hassan Msingiri, amesema kikosi hicho kinakusudia kuondoa utegemezi kutoka serikalini kwa njia ya kuwekeza katika miradi.

Commodore Msingiri aliyasema hayo jana, Makao Makuu ya KMKM Kibweni, alipokuwa akizungumza na mwekezaji Mohammed Dewji na ujumbe wake kutoka Dar es Salaam kwa lengo la kuwekeza katika kikosi hicho.

Mkuu huyo alisema lengo kubwa ni kuzalisha katika maeneo tofauti ikiwamo ya baharini ili uchumi wa bluu uanzie KMKM.

Alisema uchumi huo uanzie katika kikosi hicho kwa sababu bahari yote ipo chini ya kikosi hicho ili kwenda sambamba na sera ya uchumi wa bluu kwa vitendo na kimeshaanza taratibu za uvuvi wa maji madogo na bahari kuu.

Vile vile, alisema kikosi hicho kina miradi mingi ya ujenzi ukiwamo mradi wa kujenga chelezo ambacho hadi sasa wameshafanya utafiti wa kwanza na mwaka huu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshatoa Sh. bilioni 62 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi huo na mpango huo utakuwa kwa miaka mitatu.

Alisema kikosi hicho pia kina eneo la kujenga hoteli kubwa ya kitalii katika eneo la karibu ya kambi ya KMKM Kibweni eneo ambalo halipungui hekta zaidi ya 15, na kwamba mwekezaji huyo anakaribishwa kuwekeza katika eneo hilo.

Alisema miongoni mwa malengo ya baadaye ya kikosi hicho ni kununua meli kwa ajili ya kusafirisha abiria katika Bahari ya Hindi, lakini kusafirisha mizigo kutoka Pemba kwenda Unguja.

Naye Dewji ameahidi kuchukua maombi na mawazo ya Mkuu wa Kikosi hicho na kuyafanyia kazi kwa haraka na mingine yanaweza kuchukua muda mrefu.

Alisema katika uwekezaji wake si lazima awekeze katika kujenga viwanda ila anaweza kuweka uwekezaji wake hata kwa kutoa fedha ili kuchangia mradi husika.

Akizungumzia kuhusu kuekeza katika kampuni ya ujenzi ya KMKM alisema yupo tayari kusaidia katika maeneo yenye changamoto ili kutimiza malengo yao.

## Shinikizo la damu chanzo kifo cha wazazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Dk. Umulkurthum Omar, amesema utafiti umeonyesha ugonjwa wa shinikizo la damu ni sababu kubwa ya vifo kwa wazazi wakati wa kujifungua au baada.

Hayo aliyasema jana, Wizara ya Afya Mnazi Mmoja wakati akisoma ripoti ya utafiti kuhusu ugonjwa huo kwa wajumbe mbalimbali waliowakilisha vituo vyao vya afya.

Alisema kuwa tatizo la shinikizo la damu kuwa kubwa kwa wajawazito ni hatari na huchangia kupata kifafa cha mimba, kupoteza damu nyingi na hata kupata kilema cha kudumu kama asipopata matibabu ya haraka.

Alisema katika mwaka 2020 asilimia 28 ya vifo vya wajawazito vilichangiwa na ugonjwa wa shinikizo la damu na katika kipindi cha nyuma hali haikupishana jambo ambalo linahitaji kupatiwa mipango ya muda mrefu ya kuimarisha huduma kwa kiwango ambacho kitawasaidia kinamama hao.

Aidha, alisema bado kunahitajika elimu ya kutosha katika jamii kwa kupewa uelewa wa kuhudhuria vituo vya afya mapema wakati wa ujauzito jambo ambalo litaonyesha mwenendo wa afya na kupatiwa huduma za matibabu pamoja na kupewa ushauri nasaha.

Naye daktari Omar Mwalimu alisema matatizo ya wajawazito ni mengi na kwamba ipo haja ya kuyachukuliwa hatua ya kutoa elimu kwa jamii kuachana na imani potofu ambayo inachangia ucheleweshwaji wa mgonjwa kupatiwa huduma ya haraka.

Aliwataka wahudumu wanaoshughulikia wajawazito kuhakikisha wanatimiza majukumu yao ipasavyo ili kuwapa maelekezo na ushauri utakaowasaidia kinamama hao.

Aliwataka wahudumu wa afya kukaa karibu zaidi na jamii ili kuwapa mwongozo wa kiafya ambao utasaidia kuimarisha afya ya mjamzito na mtoto kwa kuepukana na matatizo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA YA GHOROFA INAUZWA

**Ina frem za biashara, inafaa kwa makazi, au biashara kama Guest house au Hospitali. Ipo Ukonga Dar es salaam. Simu: 0757 079057.**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## KUPOTEA KWA CHETI



**CELESTINE CHARLES MKENDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1071-0308** kilichotolewa na shule ya secondary **ST.MATHEW'S** mwaka 2014,Yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **CONTROL NAMBA 9910823973004**

116315002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JOSEPH Y GAMALIEL** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye jina **KASTORY PATRICK MPONDA** aina ya **NISSAN PIC-UP** yenye namba za usajili **T 253 DFD.**Chasis No. **UBMD22433033B,** Engine No. **TD27337521** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOM/RB/302161/2021.**

116315602

**SHERIA YA USAJILI WA ARDHI (SURA 334)**

**KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI**

**HATI NA.7799**

**MMILIKI ALIYESAJILIWA :EVANS EMMANUEL KISINANE WA S.L.P 569,MOSHI**
**MUOMBAJI:EVANS KISINANE WA S.L.P 569, MOSHI**

**ARDHI:L.O. NA.12422,FARM NO.148/2,KARANGA,MANISPAA YA MOSHI.**
**ENEO:EKARI 2.,308**

Taarifa imetolewa kwamba hati ya kumiliki ya ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na nina kusudia kutoa hati nyingine badala yake iwapo hakuna pingamizi kwa muda wa mwezi mmoja (1) tokea tarehe ya taarifa hii.

Iwapo hati ya asili itaonekana irudishwe kwa msajili wa hati msaidizi ,mkoa wa Kilimanjaro S.L.P 190 MOSHI.

(Bwigu Mohamed)
MSAJILI WA HATI MSAIDIZI
MKOA WA KILIMANJARO

116315902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 122 YA 2021**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA**
**JOSEPHINE LUINASIA MSHIU..........MAREHEMU**
**NA**
**HAIKAMEN SIMBA MSHIU...............MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa waombaji hapo.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 23 mwezi wa 06 mwaka 2021
Hati hii imetolewa 16 mwezi 06 mwaka 2021.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

116315102

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI MIRATHI**

**MIRATHI NA 52 YA MWAKA 2020**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU JEROME B LUPAPA**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**LIGHTNESS SHOO**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibituisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 23th mwezi wa JUNE mwaka 2021
Imewasilishwa Dar Es Salaam leo tarehe 17th mwezi wa MAY 2021.

NAIBU MSAJILI

116314702

## KUPOTEA KWA CHETI



**FATUMA H STAMILI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0812-0550** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya MAHIWA mwaka 2017,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DSM/PHQ/RB/142655/2021**

116314602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**STPHEN MICHAEL SIWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA PREMIO** yenye namba za usajili **T317 DSF,** engine namba **1nzb 20884** chasis namba **NZT – 2400059774.** Yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **KW/RB/1415/2021**

116316502

## KUPOTELEWA NA OFA YA KIWANJA

**TUPOKIGWE YOHAN MWAMGIGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFA YA KIWANJA CHENYE **ID 56175 NUMBER 632** LOCATION MWAKIBETE **BLOCK Y.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/300387/2021**

116314902

***Uza,***
***Chenye Thamani***
***Kubwa Kwa Kutangaza***
***Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie 0782253676***

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Baruapepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P 2888,**
**40470 DODOMA**
**Tarehe 18-06-2021**

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **IJUMAA tarehe 18-06-2021** Kampuni ya FAMARI INVESTMENT itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MTUKULA BORDER** kuelekea **DAR ES SALAAM** gari hilo lenye namba za usajili **T 561CUM / T 410DDG**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **22** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.00** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.6** |

3. Njia itakayotumika: **MTUKULA BORDER** hadi **DAR ES SALAAM kupitia BIHARAMULO,MULEBA,KAHAMA,SINGIDA, DODOMA,MOROGORO, PWANI-DAR ES SALAAM**

***Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

116316101

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Kim Jong-un akiri uhaba wa chakula nchini mwake

**Pyongyang,** KOREA KASKAZINI

KIONGOZI wa Korea Kaskazini Kim Jong-un, amekiri rasmi kuwa nchi hiyo inakabiliwa na uhaba wa chakula.

Akiwahutubia maofisa wa ngazi ya juu nchini humo, Kim alisema hali ya chakula majumbani mwa watu kwa sasa, ni ya kutia wasiwasi.

Alisema sekta ya kilimo imeshindwa kufikia malengo yake kutokana na tufani ya mwaka jana iliyosababisha mafuriko.

Kuna ripoti kwamba bei ya chakula imepanda, huku shirika la habari la Korea Kaskazini likiripoti kilo moja ya ndizi inagharimu dola 45 za Kimarekani.

Korea Kaskazini imefunga mipaka yake ili kudhibiti kuenea kwa virusi vya Covid-19.

Biashara kati yake na China, imeporomoka sana kutokana na hatua hiyo.

Korea Kaskazini inategemea China kwa chakula, mbolea na mafuta.

Korea Kaskazini pia inalemewa na vikwazo vya kimataifa, vilivyowekwa kwa sababu ya mipango yake ya nyuklia.

Kiongozi huyo wa kimabavu wa serikali ya chama kimoja, alizungumzia hali ya chakula katika mkutano wa kamati kuu ya Chama cha Wafanyakazi, ambayo ilianza wiki hii katika mji mkuu Pyongyang.

Hadi sasa, Korea Kaskazini, inadai kuwa kufunga mipaka yake kumefanya waepuke kuenea virusi vya corona, ingawa wachambuzi wanatilia shaka madai hayo.

**BBC**

## Wanajeshi 20 wauawa Afghanistan

**Faryab,** AFGHANISTAN

MAOFISA wa mkoa wa Kaskazini wa Faryab wamesema kundi la Taliban limewaua zaidi ya makomando 20 wa jeshi.

Kulingana na madiwani wa mkoa huo, wanajeshi kutoka kikosi maalumu walipelekwa katika mkoa kuikomboa wilaya iliyotekwa na Wataliban takriban siku 10 zilizopita.

Madiwani hao, Abdul Manan Qati na Fazal Haq Mohammadi, walisema vikosi vya usalama vilichukua udhibiti wa wilaya ya Dawlat Abad kutoka kwa Taliban Jumanne wiki hii, jioni, ingawa wapiganaji waliokuwa wamejificha katika vijiji vya jirani wakafanya shambulio la kuvizia.

Vifaru vya kijeshi visivyopungua viwili, viliharibiwa katika milipuko ya mabomu ya kandoni mwa barabara wakati wa shambulio hilo.

Vurugu zinaendelea bila ukomo ingawa, tangu kuanza rasmi kwa mchakato wa kuondoa wanajeshi wa Marekani na NATO, Mei Mosi, mwaka huu, wilaya zisizopungua 27 zimeangukia mikononi mwa kundi la Taliban.

**DW**

# Mwendesha Mashtaka ICC aapa kushughulikia wahalifu

**The Hague,** UHOLANZI

KARIM Asad Ahmad Khan ameanza rasmi kuhudumu kama Mwendesha Mashtaka Mkuu mpya wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC).

Karim Asad Ahmad Khan, ambaye ni wakili kutoka Uingereza, alikula kiapo katika jengo la ICC, The Hague, Uholanzi, mbele ya Rais wa Mahakama hiyo, Jaji Piotr Hofmanski, na kuanza rasmi jukumu lake la kuhudumu miaka tisa.

Katika hotuba yake baada ya sherehe ya kuapishwa, Khan alibainisha kuwa atafanya kazi kuhakikisha kuwa wahalifu hawaachi bila kuadhibiwa na kwa hivyo, atachukua hatua kulingana na makubaliano ya uanzishaji wa mahakama na Sheria ya Roma.

Alisema kuwa kama ofisi ya mwendesha mashtaka, wanapaswa kuahidi mengi na sio kuwarudisha mikono mitupu kutoka kortini, pia alisema watachukua hatua kulingana na uadilifu.

Khan, ambaye alikuwa mkuu wa timu ambayo hivi karibuni ilifanya uchunguzi juu ya mauaji ya kimbari, uhalifu dhidi ya ubinadamu na uhalifu wa kivita wa shirika la kigaidi la DEASH nchini Iraq kwa niaba ya Umoja wa Mataifa (UN).

Alitambulika sana mara ya kwanza mwaka 2014, wakati Israel iliposhambulia Gaza na Marekani ilipotangazwa kupitia uchunguzi juu ya uhalifu wa kivita huko Afghanistan.

Wakati huo huo, Fatou Bensouda, ambaye muhula wake wa kuhudumu kama Mwendesha Mashtaka Mkuu wa ICC ulimalizika juzi, alitoa ujumbe wa kuaga.

Bensouda, kwenye mkutano wa kumuaga uliofanyika kwa ajili yake alisema, "Ili kuwa na haki, ufanisi na uzuiaji, ofisi ya mwendesha mashtaka lazima iamue kwa msingi wa sheria peke yake, bila woga na bila upendeleo wala kujali."

Bensouda, alianza jukumu lake kama Mwendesha Mashtaka Mkuu, Juni 15, mwaka 2012 kupitia kura za chama cha mamlaka za ICC, alifanya maamuzi muhimu kuhusu Afghanistan, Palestina, Ukraine na Myanmar wakati wa kipindi chake cha uongozi.

Bensouda alikuwa chini ya vikwazo vya visa vya Marekani chini ya uongozi wa Rais wa zamani Donald Trump kwa kuchunguza iwapo wanajeshi wa Marekani walifanya uhalifu wa kivita huko Afghanistan.

**TRT**



Rais wa zamani wa Ivory Coast, Laurent Gbagbo, amerejea nchini Ivory Coast jana, kwa mara ya kwanza katika kipindi cha takriban muongo mmoja, baada ya kuishi Brussels tangu Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) kumwacha huru mwaka 2019. **PICHA: DW**

# Ggabgo arejea nyumbani baada ya muongo mmoja

**Abidjan,** IVORY COAST

RAIS wa zamani wa Ivory Coast Laurent Gbagbo amerejea nchini hapo jana, kwa mara ya kwanza tangu alipokamatwa na kufikishwa mbele ya Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Jinai (ICC), Novemba mwaka 2011.

Hiyo ilitokana na jukumu lake katika ghasia za baada ya uchaguzi, ambazo zilisababisha vifo vya maelfu ya watu. tovuti ya Koaci, iliripoti. Ndege ya Gbagbo kutoka Brussels inatarajiwa kutua mjini Abidjan saa tisa alasiri, jana.

Mamlaka za Ivory Coast ziliahidi kwamba, atapokelewa kwa heshima zote kutokana na hadhi ya ofisi aliyowahi kushikilia.

Kurejea kwa Gbagbo, kunatarajiwa kupiga jeki chama chake cha Ivorian Popular Front, ambacho kinakabiliwa na mgawanyiko kwa miaka kadhaa sasa.

Waathiriwa wa ghasia za baada ya uchaguzi, waliapa kufanya maandamano atakaporejea.

Ijapokuwa Gbagbo aliondolewa, mashtaka yote katika kesi dhidi yake ya ICC, Machi 31, mwaka huu, bado anakabiliwa na mashtaka kwa kuhusika na wizi katika Benki Kuu ya taifa hilo la Afrika Magharibi tawi la Abidjan (BCEAO).

Alihukumiwa kifungo cha miaka 20 jela kwa kuhusika na wizi wa BCEAO, Januari mwaka 2018.

Rais Ouattara, alimsamehe katika kesi hiyo, ingawa hakuwajumuisha watu waliofunguliwa mashtaka katika mahakama za kimataifa.

**BBC**



# MANCINI

## ITALIA IKITINGA MTOANO EURO

**ROME, Italia**

ROBERTO Mancini amesema Domenico Berardi na Manuel Locatelli, walifanya "kile ambacho mara zote nawaambia wakifanye" kwa muunganiko wao wakati Italia ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Uswisi, juzi Jumatano usiku.

Matokeo hayo ambayo yalikuja baada ya Locatelli kufunga mabao mawili na Ciro Immobile kufunga la tatu, yaliithibitisha Italia kutinga hatua ya mtoano kwenye michuano ya Euro 2020 baada ya kucheza mechi mbili.

Vijana hao wa Mancini walitawala mchezo huo uliopigwa kwenye dimba la Olimpico na walipata ushindi wa pili mfululizo wa mabao 3-0, wakitoka kuwafunga Uturuki idadi kama hiyo katika mchezo wa ufunguzi wa Kundi A.

Mancini alikisifia kiwango cha wachezaji wake, akiwaambia waandishi wa habari: "Uswisi ni timu ngumu. Tulijua kwamba utakuwa mchezo mgumu na ndivyo ilivyokuwa.

"Tulitengeneza nafasi kadhaa na tulistahili ushindi. Tulikuwa kwenye wakati mgumu dakika za mwanzo, lakini baadaye tukasukumiza mashambulizi kwa kasi na kuwasababisha wao wafanye makosa.

"Kwa hakika vijana walifanya vizuri. Haikuwa rahisi; ulikuwa mchezo wao wa pili ndani ya siku tano."

Italia ilianza kupata bao la kwanza kupitia kwa Locatelli kabla ya baadaye kucheza vizuri na Berardi na yeye kufunga la pili.

"Hivyo ndivyo mara zote ninavyowaambia nini cha kufanya. Leo (juzi) wamefanya kile ambacho mara zote nawaambia wakifanye," alisema Mancini.

## LUKAKU AMEIVA TATIZO NI UTOTO - MOURINHO

**LONDON, England**

JOSE Mourinho amesema kwamba, Romelu Lukaku sasa ni mchezaji aliyeiva vizuri zaidi na kwamba, akiwa Manchester United alikuwa akijifunza.

Mourinho ambaye alifukuzwa kule Tottenham Hotspur Aprili mwaka huu na mwezi uliopita akatangazwa kuwa kocha mpya wa AS Roma, amekuwa akiwazungumzia wachezaji aliowanoa ambao wapo kwenye michuano ya Euro 2020 inayoendelea.

Kwa sehemu kubwa amekuwa akiwazungumzia wachezaji wa Man United na timu ya Taifa ya England, Luke Shaw, Marcus Rashford, Kyle Walker na sasa Lukaku.

Lukaku alisajiliwa na United akitokea Everton mwaka 2018 kwa dau la pauni milioni 75.

Ndani ya miaka minne aliyokaa pale Old Trafford, Lukaku alikuwa na kiwango cha kupanda na kushuka kabla ya kujiunga na Inter Milan ambako ameenda kuwa muhimili mkubwa wa timu hiyo kwa miaka miwili ambayo amekuwapo klabuni hapo.

Ameisaidia Inter kutwaa ubingwa wa Serie A kwa kuwavua ubingwa Juventus ambao walikuwa watawala kwa miaka tisa mfululizo.

Katika moja ya uchambuzi wake kwenye televisheni, Mourinho amesema; "Lukaku alipokuwa Chelsea alikuwa ni mtoto, alipokuwa Manchester United alikuwa bado anajifunza, lakini akiwa Inter amekuwa mchezaji kamili.

"Miaka miwili ndani ya Inter imempa uwezo binafsi wa kujiamini, kitu ambacho hakuwa nacho hapo awali.

"Anapendwa na mashabiki, wachezaji wenzake, kocha na benchi la ufundi. Ni mchezaji mkubwa, lakini ana utoto ndani yake. Anahitaji kupendwa, kusaidiwa na kujisikia ni wa muhimu."



# VARANE AMSIFIA POGBA UFARANSA

**MUNICH, Ujerumani**

RAPHAEL Varane amemsifia Paul Pogba kuwa ni kiungo aliyekamilika baada ya kung'ara kwenye mchezo wa kwanza wa ufunguzi wa michuano ya Euro 2020 dhidi ya Ujerumani.

Kikosi hicho cha kocha, Didier Deschamps ambacho ni Mabingwa wa Dunia, walianza mchezo wao wa Kundi F kwa ushindi wa bao 1-0 mjini Munich, Jumanne baada ya Mats Hummels kujifunga.


Ufaransa pia walipata mabao mawili ambayo yalikataliwa kwa sababu wafungaji walikuwa wameotea.

Bao hilo la Ufaransa lilipatikana baada ya juhudi binafsi za Pogba, ambaye alimpasia Lucas Hernandez na katika harakati za kukoa Hummels akajikuta anausindikiza mpira kwenye nyavu za goli lake.

Akicheza kama winga wa kulia pamoja na Adrien Rabiot na N'Golo Kante, Pogba alitengeneza pasi 52 zikiwa nyingi zaidi kuliko mchezaji yeyote katika kikosi cha Ufaransa, huku 40 zikifika eneo husika kwa usahihi sawa na asilimia 76.9. Aligusa mpira mara 78 na pia alikuwa mchezaji aliyefanyiwa faulo nyingi zaidi (nne) kwa kikosi cha Ufaransa.

"Alianza kwa morali kubwa zaidi, anacheza akiwa mchezaji aliyepevuka zaidi, ana ubora mwingi sana," alisema Varane akimzungumzia Pogba.

## HABARI MICHEZO




# DEMBELE, BARCA MAMBO MAGUMU

**BARCELONA, Hispania**

MAZUNGUMZO ya kuongeza mkataba mpya kati ya wababe wa Hispania, Barcelona na winga Ousmane Dembele, yamekumbana na kikwazo, kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari nchini humo.

Mfaransa huyo, ambaye kwa sasa yuko katika majukumu ya kitaifa kwenye Euro 2020, mkataba wake wa sasa unamalizika Juni 2022, na klabu hii ya Catalunya haitaki kuona nyota huyu mwenye umri wa miaka 24 anaondoka kama mchezaji huru.

Kwa mujibu wa Marca, ikiwa Barcelona watashindwa kukubaliana na Dembele kuongeza mkataba mpya, basi wataangalia uwezekano wa kumuuza winga huyo kwenye dirisha hili kubwa la usajili la majira ya joto.

Dembele ataweza kujadiliana na klabu nyingine kuanzia Januari 2022 kama atakuwa hajafikia makubaliano ya kuongeza mkataba mpya hapo Camp Nou.

Barcelona ilimsaini Mfaransa huyo kutoka Borussia Dortmund ya Ujerumani, Agosti 2017 kwa pauni milioni 90 na nyongeza ya pauni milioni 34.

Dembele amefunga mabao 30 na kutoa pasi za mwisho 21 katika mechi 118 hapo Barcelona, pamoja na mabao 11 na asisti tano kwa msimu huu unaomalizika wa 2020-21.

# ARSENAL KUPOTEZEA KUMREJESHA RAMSEY

**LONDON, Rngland**

ARSENAL wanatajwa kuwa hawatazamii kumrudisha, Aaron Ramsey pale kwenye Uwanja wa Emirates akitokea Juventus msimu huu wa majira ya joto.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales, anaaminika kutaka kurudi kwenye Ligi Kuu England, miaka miwili baada ya kuondoka kule London Kaskazini kwenda Turin.

Ramsey hapo awali alikuwa na Arsenal kwa misimu 11, kabla ya kuondoka kwa uhamisho wa bure, lakini wakati wake huko Juve haujaenda kama alivyotarajia.

Mfululizo wa changamoto ya majeraha umeathiri kampeni mbili za nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, na Juventus inatajwa kuwa tayari kumweka sokoni.

Arsenal ni moja ya timu zinazohusishwa na nyota wao wa zamani, lakini Goal.com inadai kuwa "hakuna nafasi" kwa 'Washikabunduki' hao kutoa ofa.

Liverpool pia inaaminika ilionyesha nia kwa Ramsey, ambaye alifunga mabao mawili na kusaidia mengine manne katika mechi 22 za Serie A msimu uliopita.




# SPURS YAIPIKU LIVER KWA PELLEGRINI

**LONDON, England**

TOTTENHAM Hotspur imeripotiwa kuwa mbele ya wapinzani wao kwenye Ligi Kuu England, Liverpool katika mbio za kuwani kumsajili kiungo wa AS Roma, Lorenzo Pellegrini.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, anamaliza mkataba pale katika dimba la Olimpico mwakani, ikimaanisha kuwa Roma wanaweza kulazimika kumuuza katika msimu huu wa joto ikiwa mkataba mpya hautakubaliwa.

Spurs, ambao hivi karibuni watangaza uteuzi wa bosi wa zamani wa Roma, Paulo Fonseca, wanaaminika kuwapiku Liverpool na miamba ya LaLiga, Barcelona kuwania saini ya Pellegrini.

Kwa mujibu wa Calciomercato, Spurs wameonyesha nia zaidi ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia na wako tayari kulipa Euro milioni 30, badala ya kujadiliana na Roma.

Pellegrini alifurahia msimu wa 2020-21 kwa upande wa Italia, akifunga mara 11 na kusajili pasi za mwisho tisa katika mechi 47 kwenye mashindano yote.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RAMOS AONDOKA RASMI REAL MADRID

## Beki huyo sasa amegeuka lulu Ulaya na huenda akatua PSG, Manchester ama...

**MADRID,** Hispania

GWIJI wa Real Madrid na beki mkongwe wa Hispania, Sergio Ramos, ameondoka rasmi katika klabu hiyo jana, Alhamisi.

Miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, walithibitisha na kumuaga mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa mwezi huu.

Na hiyo imehitimisha kipindi cha miaka 16 ya mlinzi huyo cha kucheza pale 'Los Blancos'.

**Ramos aliripotiwa kwamba, yupo tayari kuongeza mkataba mpya wa kukaa klabuni hapo, lakini majadiliano yalishindwa kufikiwa.**

Mkongwe huyo alikuwa anataka mkataba mpya wa miaka miwili ili kuendelea kukaa hapo Bernabeu, lakini Madrid walikuwa tayari kumpa mwaka mmoja tu.

Ramos alicheza mechi 15 za LaLiga msimu wa 2020-21, na hilo lilitokana na kukumbwa na majeraha ya mara kwa mara.

Aliachwa kwenye kikosi cha Hispania kinachoshiriki michuano ya Euro 2020 kutokana na kutokuwa fiti, akisumbuliwa na kigimbi cha mguu pamoja na goti.

Ramos aliwasili hapo Bernabeu kutoka Sevilla mwaka 2005, akiwa na umri wa miaka 19 wakati aliporithi jezi ya gwiji, Fernando Hierro.

Ameshinda mataji matano ya LaLiga na mawili ya Copa del Rey [Kombe la Mfalme] kwa kipindi alichokaa klabuni hapo, akibeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nne.

Pia alishinda taji la Super Cup mara nne, Kombe la Ulaya mara tatu na Klabu Bingwa Dunia mara nne

Beki huyo sasa amegeuka lulu Ulaya na huenda akatua katika moja ya klabu za Paris St-Germain, Manchester City, Manchester United na Sevilla.

## KWA UFUPI

**WHITE AOTA MBAWA ARSENAL**

KLABU ya Brighton imekataa dau la pauni milioni 40 kutoka Arsenal kwa ajili ya mlinzi wa England, Ben White mwenye umri wa miaka 23. Mlinzi huyo ameichezea Brighton mechi 36 za Ligi Kuu England msimu uliopita na kufanikiwa kuitwa timu ya Taifa ya England. (***Sky Sports***)

**ODEGAARD KUBAKI MADRID**

ARSENAL imerudi nyuma kuhusu mpango wao wa kumsajili nyota wa kimataifa wa Norway, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 22, hivyo kiungo huyo anatarajiwa kusalia klabuni kwake Real Madrid baada ya kutumia sehemu ya pili ya msimu akiwa kwa mkopo hapo Emirates. (**AS**)

**COMAN ANAITAKA EPL**

WINGA wa Ufaransa, Kingsley Coman mwenye umri wa miaka 25, anataka kuhamia Ligi Kuu England baada ya kugoma kusaini mkataba mpya kule Bayern Munich. (**Sky Sports**)

**INTER YAMWANIA DUMFRIES**

INTER Milan inajiandaa kupambana na Everton katika mbio za kuwania saini ya mlinzi wa Uholanzi, Denzel Dumfries mwenye umri wa miaka 25, kutoka PSV Eindhoven. (**Voetbal International**)

**GONZALEZ HUYO BRIGHTON**

KLABU ya Brighton imekubaliana na Stuttgart katika uhamisho wa pauni milioni 25 kwa ajiili ya mshambuliaji, Nicolas Gonzalez mwenye umri wa miaka 23 raia wa Argentina, ambaye amepachika mabao sita katika michezo 15 ya Ligi Kuu Ujerumami, Bundesliga, msimu wa 2020-21. (**Guardian**)

**SPURS YAMTAKA LAMPTEY**

KLABU ya Tottenham Hotspur inamtaka mlinzi wa kulia wa Brighton na timu ya Taifa ya England chini ya miaka 21, Tariq Lamptey mwenye umri wa miaka 20, ambaye ameng'ara msimu uliopita akiwa na kikosi hicho cha kocha Graham Potter, kabla ya kupata majeraha Desemba yaliyomweka nje ya uwanja hadi mwisho mwa msimu. (**Sky Sports**)

**WELBECK ATAKIWA BRIGHTON**

KLABU ya Brighton ipo kwenye mazungumzo na nyota wa zamani wa England, Danny Welbeck mwenye umri wa miaka 30 kuhusu mkataba mpya. (**The Argus**)

**KANE MAMBO MAGUMU**

MATUMAINI ya mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27 ya kutimka Tottenham Hotspur kuelekea kwa mabingwa wa Ligi Kuu England, Manchester City yanakutana na ugumu kutokana na klabu hizo kupangwa kucheza mechi ya kufungua pazia la Ligi Kuu 2021-22. (***The Telegraph***)

**BERGE ANUKIA ARSENAL**

KLABU ya Sheffield United huenda ikalazimika kukubali dau la Arsenal kwa ajili ya kiungo wake kutoka Norway, Sander Berge. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, anasema anamatumaini kwamba atacheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. (***Sheffield Star***)

**ALIOSKI KUONDOKA LEEDS**

LEEDS United haijakata tamaa ya kumshawishi, Ezgjan Alioski mwenye umri wa miaka 29, kuendelea kusalia hapo kwenye dimba la Elland Road. Winga huyo wa Macedonia anatarajia kutimka kama mchezaji huru msimu huu baada ya kushindwa kuafikiana kuhusu mkataba mpya, akionekana kupunga mkono wa kwa heri katika siku ya mwisho ya msimu. (***Mirror***)

# TSHABALALA AANZA MAZOEZI WIMBO WA UBINGWA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA msaidizi wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', amesema tayari ameanza mazoezi ya wimbo wake wa kila mwaka wakati klabu yake ikitwaa ubingwa, ili auimbe tena wakati wakibeba taji hilo msimu huu. Beki huyo wa kulia amesema kwa hali ilivyofikia wanaona wako karibu kabisa kuuchukua ubingwa kwa mara ya nne mfululizo.

Tshabalala alisema hayo, akizungumzia maandalizi ya mchezo wao wa kesho Jumamosi dhidi ya Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza.

**"Ubingwa ndiyo malengo yetu. Tulikuwa kwenye mapumziko ya mechi za timu za taifa zilizo kwenye Kalenda ya FIFA. Tumemaliza na sasa tunakwenda kuwania ubingwa wetu," alisema mchezaji huyo.**

Alisema yeye na wenzake kama kawaida wamejiandaa kukabiliana na mechi hiyo na malengo ni kupata ushindi kila mchezo ili wahifadhi tena taji lao kwa mara nyingine.

Mchezaji huyo aliongeza kuwa atawaongoza tena wachezaji wenzake kuimba wimbo wake maarufu wa 'Tutachukua tena', wakati wakitawazwa kuwa mabingwa.

"Naamini hivyo kwa sababu Simba ina kikosi kizuri, viongozi wanajitahidi sana kuiandaa timu ndiyo maana nina imani hiyo, na hata msimu uliopita wakati naimba nilisema mwakani tutachukua tena kwa sababu nilikuwa na uhakika,"alisema.

Kwa misimu mitatu mfululizo Simba imechukua ubingwa ambao mara nyingi huwa unachagizwa na wimbo ambao huimbwa na wachezaji wa timu hiyo, wakiongozwa na Tshabalala mwenyewe ambaye hushika kipaza sauti wakati wakiwa kwenye gari la wazi na kombe lao.

Baadhi ya maneno ambayo huimbwa ni "Tulichukua tena, tumechukua tena na mwakani tutachukua tena."




Mmoja kati ya wachezaji wa gofu akicheza katika moja ya mashindano yaliyoandaliwa na kinywaji cha Johnnie Walker hivi karibuni katika viwanja vya Lugalo. **MPIGAPICHA WETU**

# Johnnie Walker bega kwa bega na Gofu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia kinywaji chake cha Johnnie Walker, imesema itaendelea kusaidia maendeleo ya mchezo wa gofu hapa nchini.

Meneja masoko wa vinywaji vikali wa kampuni hiyo, Minga Lumuli, amesema kinywaji cha Johnnie Walker ni mdau wa maendeleo ya mchezo na kwamba tayari imeshakuwa moja kati ya wadau wakubwa wa mchezo wa gofu.

"Gofu ni moja kati ya michezo ambayo inakuwa kwa kasi hapa nchini na Johnnie Walker inayofuraha kubwa kutoa mchango wake katika kusaidia maendeleo yake," alisema Lumuli.

Gofu ni moja kati ya michezo yenye historia kongwe duniani. Mchezo huu ulianza takriban miaka 600 iliyopita na kwa sasa unakuwa kwa kasi huku ukichezwa na watu wa kariba tofauti tofauti.

Mchezo huu pia umekuwa ukitoa mchango mkubwa wa kiuchumi kupitia ajira kwa vijana wanaofanya kazi katika viwanja vyake pamoja na kukuza na kutanga utalii kupitia wageni wanaokuja na kuucheza nchini.

Lumuli alisema: "Johnnie Walker ni kinywaji cha kimataifa chenye chimbuko lake nchini Scotland na pia kinasherehekea pia miaka 200 tangu kuanza kutengenezwa na kufanya kuwa moja ya kinywaji chenye historia kongwe duniani kama ulivyo mchezo wa gofu."

Lumuli anaongea kuwa kwa sasa kinywaji hicho kinadhamini mashindano katika klabu maarufu za gofu hapa nchini ikiwa ni pamoja na Dar es Salaam na Arusha Gymkhana Club, Lugalo Gofu Club pamoja na Sea Cliff Golf Club ya Zanzibar.

Mmoja wa wachezaji gofu wakongwe, Dismas Lyakato, amesema kuingia katika kudhamini mashindano ya gofu, kinywaji cha Johnnie Walker kimeongeza ubora wa mashindano na pia kuvutia vipaji vipya katika mchezo huu.

Alisema gofu ni mchezo ambao ulikuwa haupewi kipau mbele sana kwenye suala la udhamini kama ilivyo mchezo wa mpira wa miguu na kwa maana hiyo, umekuwa haukuwi kwa haraka lakini kuha kwa Johnnie Walker kumeunyanyua na sasa unaenda vizuri.

Kampuni ya Bia ya Serengeti ni mdau wa michezo mingine ikiwamo mpira wa miguu. SBL ndiyo mdhamini wa timu ya Taifa, Taifa Stars na pia ndiyo mdhamini wa kwanza na wa pekee kwa Ligi Kuu ya Wanawake nchini.

# Katwila na matumaini Ihefu kubaki Ligi Kuu

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya kupokea kipigo cha mabao 2-0 ugenini dhidi ya JKT Tanzania juzi, Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila, amesema bado ana matumaini makubwa ya kuibakisha timu hiyo Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Matokeo hayo yanaifanya Ihefu kutokuwa sehemu salama kwani nafasi ya 14 iliyopo na pointi zake 34, kunailazimu kushinda mechi zake tatu zilizosalia ili kujihakikishia kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila alisema wachezaji wake walipata nafasi nyingi katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, lakini walishindwa kuzitumia na kujikuta hadi dakika 90 zinamalizika wakitoka patupu.

"Bado tuna matumaini ya kuendelea kubaki Ligi Kuu, nitayafanyia kazi makosa madogo madogo niliyoyabaini katika mchezo wetu uliopita ili niweze kufanya vizuri kwenye mchezo ujao," alisema Katwila ambaye timu yake itashuka tena dimbani Jumapili katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoka dhidi ya Kagera Sugar iliyopo nafasi ya 11 ikiwa na pointi 36 zilizotokana na mechi 31.

# Mo aahidi makubwa kwa KMKM ya Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** Zanzibar

MWEKEZAJI na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu ya Simba, Mohamed "Mo" Dewji, ameahidi kuwapiga tafu mabingwa wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM ikiwa ni pamoja na kutoa ushirikiano na uzoefu wa kiuongozi kwa klabu hiyo.


Akizungumza na gazeti hili Katibu Mkuu wa KMKM, Sheha Mohamed, alisema Mo alitoa kauli hiyo baada ya kuitembelea klabu hiyo Jumanne wiki hii.

Alisema Mo ameahidi kuisaidia timu hiyo katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha timu hiyo inapiga hatua katika ngazi ya uongozi na timu yenyewe kwa ujumla.

Sheha alisema kitendo cha KMKM kupata fursa ya kuanzisha ushirikiano na mtu kama Mo ni bahati kwao kwa kuwa yeye ni mwekezaji, hivyo anaimani timu hiyo inaweza kupiga hatua katika soka la Zanzibar.

"Viongozi wa KMKM tumefarijika na tunaona kuwa ni bahati kutembelewa na mwekezaji na mfanyabiashara mkubwa, hii kwetu ni fursa, kikubwa maeneo gani ambayo atatoa ushirikiano zaidi hatua hii itafuata baada kukaa meza moja na kufikia makubaliano," alisema.

Michezo
Ijumaa Juni 18, 2021
Nipashe



RAMOS AONDOKA RASMI MADRID

HABARI UK 22




Kiungo wa Wales, Aaron Ramsey, akiifungia timu yake bao la kwanza wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Uturuki kwenye mechi ya michuano ya Euro 2020 iliyopigwa Uwanja wa Baku Olympic, Azerbaijan juzi. **PICHA: MTANDAO**

## TSHABALALA ATUNGA WIMBO WA UBINGWA



**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA msaidizi wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', amesema tayari ameanza mazoezi ya wimbo wake wa kila mwaka wakati klabu yake ikitwaa ubingwa, ili auimbe tena wakati wakibeba taji hilo msimu huu.

Beki huyo wa kulia amesema kwa hali ilivyofikia wanaona wako karibu kabisa kuuchukua ubingwa kwa mara ya nne mfululizo.

UK. 23

# MAYAY ATOA SABABU KUKUBALI KUKATWA TFF

**Aonyesha uanamichezo, akiri kutotimiza vigezo huku akiahidi kuendelea kusaidia...**

**Na Saada Akida**

HATIMAYE aliyekuwa mgombea wa nafasi ya urais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Ally Mayay, amekiri kuwa mpole na kuweka 'silaha' chini za kutopinga maamuzi ya kuenguliwa kwake katika mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa shirikisho hilo unaotarajiwa kufanyika Agosti 7, mwaka huu jijini Tanga.

Kamati ya Uchaguzi ya TFF, juzi ililiengua jina la Mayay huku Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Benjamin Kalume, akieleza kuwa ni kutokana na kutotimiza vigezo vya kanuni ikiwamo kutokuwa na wadhamini watano na pia kutowakilisha vyeti vyake vilivyoidhinishwa na mamlaka ya viapo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, Mayay alitoa sababu iliyomfanya kuridhika na uamuzi huo wa kuenguliwa akieleza kuwa ni kutokana na ukweli kwamba hakutimiza vigezo vya kanuni ikiwamo idadi ya 'Endorsement' (wadhamini) na kutopeleka nakala ya vyeti vilivyoidhinishwa kwa muhuri na mamlaka ya viapo, hivyo haoni sababu ya kutaka kuchelewesha mchakato huo na badala yake anabariki uendelee.

Alisema kutokana na kuona soka la Tanzania linapiga hatua, hatachukuwa hatua yoyote kwa ngazi nyingine na badala yake kuuacha mchakato huo uendelee kwa mujibu wa ratiba ilivyopangwa na kamati hiyo ya uchaguzi.

"Ni kweli kuna vitu sikuambatanisha 'copy' (nakala) ya vyeti vyangu, badala yake nilikuwa nina halisi, ila sikuona umuhimu wake, yote kwa yote nakubaliana na hatua hiyo na sitachukuwa hatua yoyote.

"Si lazima niwe kiongozi, nitaendelea kutoa mchango wangu kwa kushauri kama ilivyo mdau wa soka na nafasi zangu ambazo naongoza katika vyama vingine ikiwamo mjumbe wa mkutano mkuu kwenye Chama cha Wachezaji wa Kulipwa Tanzania (SPUTANZA).

"Katika uchaguzi kuna changamoto nyingi sana ikiwamo nilizokutana nazo kwenye chaguzi zote mbili ikiwamo kuondolewa katika kugombea SPUTANZA kwa sababu ya kutokuwa na stakabadhi ya malipo ya uanachama," alisema Mayay.

Alisema kwa SPUTANZA, alishangazwa na kudaiwa stakabadhi za malipo ya ada ilhali walikuwa na makubaliano na Mwenyekiti wao, Mussa Kisoky na Katibu wake, Said George, kuhusu malipo ya ada kwa fedha ambazo amezichangia wakati chama hicho kikihitaji fedha.

"Kwa changamoto iliyojitokeza kwa upande wa SPUTANZA, imekuwa somo kwangu kuhakikisha nitalipa ada zangu zote, kuhusu Uchanguzi wa TFF, nitabaki kutoa ushauri na maoni yangu kwa wagombea.

"Jambo ambalo nitawashauri wagombea, la kwanza kuongeza idadi ya wanachama iwe zaidi kwa kuwapa nafasi vyuo vikuu hii ni kuwapa nafasi ya utafiti wowote kuhusu michezo na benki ambazo zitasaidia katika masuala ya fedha," alisema Mayay.

Alisema lingine ni pamoja na kuwapo kwa mjadala mrefu wa kitaifa hasa kanuni za katiba zinapotoka ili kuweza kupata hoja na kufanyiwa kazi ili mambo kama hayo yasijitokeze tena.

Alisema wale ambao walimuunga mkono kuwania nafasi hiyo waendelee kumsapoti hasa kipindi chote ambacho atakuwa mshauri na kuhitaji kuona soka la Tanzania likisonga mbele.

Mbali na Mayay, wengine waliokosa sifa ya kuendelea katika mchakato huo wa uchaguzi kati ya sita waliochukua na kurejesha fomu kwa nafasi ya urais ni Oscar Oscar na Ally Saleh huku waliopenya baada ya kukidhi vigezo hivyo wakiwa ni Hawa Mniga, Evans Mgeusa na Wallace Karia, anayetetea kiti chake.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Kalume, kuanzia kesho Juni 19 hadi 21 ni kipindi cha kuweka na kuwekewa pingamizi kwa waliopita katika mchakato na baada ya hapo Juni 22 hadi 24 ni kusikiliza pingamizi hizo na Juni 25 hadi 27, mwaka huu ni kipindi cha kufanya usahili.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002